# Nipashe

Jumanne Julai 12, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581004

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ



BREAKING NEWS

JACKPOT BABA LAO!

281,620,910/-

KWA 1000/- TU!

SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#




**Mtuhumiwa** ujambazi sugu auawa akijaribu kuwatoroka polisi

UKURASA 8




MANCHESTER UNITED SASA KUMTEMA RONALDO

UKURASA 21



# Halmashauri Jiji zabanwa

• **Mkurugenzi**, wengine 9 wasimamishwa kazi... *Ukurasa 2,3*

## YALIYOMO


UKURASA WA 5

**UHUSIANO TANZANIA, BENKI YA DUNIA WAIMARIKA**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba amesema kuwa uhusiano kati ya...

UKURASA WA 5

**UNFPA YAONA ONGEZEKO LA WATU, UKATILI KIJINSIA**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA), limesema kuwa...

UKURASA WA 9

**KAIRUKI YAWEKA KAMBI KUTOA ELIMU AFYA AKILI**

IDARA ya Ustawi wa Jamii ya Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU) kwa...





Ofisa Mkuu wa Teknolojia na Mabadiliko ya Kidijitali wa NMB, Kwame Makundi, akimkabidhi Tuzo ya Uongozi wa Biashara barani Afrika mwaka 2022, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna aliyotunukiwa na Jarida la African Leadership katika hafla iliyofanyika jijini London juzi. Tuzo hiyo imemtambua Zaipuna kuwa kiongozi shupavu na mahiri kwa uongozi wake na ubunifu katika sekta ya benki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Magari 1,000 yafungwa mfumo wa gesi

UKURASA 4

## Mjadala wa nauli ATCL China wamwibua balozi

UKURASA 2


**MICHEZO** YANGA KUWEKA MIKAKATI KIMATAIFA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA



Maofisa wa IPP Media wakiwa pamoja na maofisa wa Kampuni ya Dentsu Aegis Network Tanzania baada ya mkutano wa kibiashara uliofanyika jijini Dar es Salaam jana. Kutoka kushoto ni Mkurugenzi wa Biashara wa The Guardian Ltd, Ajay Goyal, Meneja wa Fedha wa Dentsu Aegis Network Tanzania, Bernard Mshana (wa tatu kushoto), Mshirika wa Vyombo vya Habari, Issack Noah (wa nne kushoto), Mkurugenzi wa The Guardian Ltd Joyce Luhanga (wa tano kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa Dentsu Aegis Network Tanzania, Edward Shila (wa nne kulia), Meneja Matangazo wa The Guardian Ltd, Angel Navuri, Meneja Masoko wa EATV & EA Radio, Roy Mbowe (wa pili kulia) na Meneja Uhusiano wa IPP Media, Nancy Mwanyika. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Halmashauri zabanwa makusanyo ya fedha

**Na Mwandishi Maalum**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewaagiza viongozi wa mkoa wa Dar es Salaam, kuhakikisha makusanyo ya fedha za ndani yanatumika kwenye ujenzi wa miradi ya maendeleo, badala ya kutegemea fedha zinazotoka Serikali Kuu pekee.

Waziri Mkuu alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam, katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, katika ziara ya kikazi kukagua shughuli za maendeleo.

"Mwaka 2020/2021 mlikusanya zaidi ya Sh. bilioni 40, pamoja na makusanyo hayo makubwa, lakini hatuoni mradi mkubwa unaotekelezwa kupitia fedha hizo. Makusanyo ya mapato na matumizi yasimamiwe vizuri na fedha hizo zitumike katika ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo," alisisitiza.

Katika ziara hiyo yenye lengo la kukutana na viongozi na watumishi wa umma mkoani Dar es Salaam, ni kuwakumbusha wajibu wao na kuwahamasisha kufanya kazi wa bidii, kusimamia vizuri maeneo yao na wafanye kazi kwa weledi na uaminifu mkubwa.

Kauli ya Waziri Mkuu inakuja baada ya Juni 17, mwaka huu, Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo, kuitaka serikali kuzibana halmashauri zenye matumizi makubwa kiasi cha kugawana fedha kwenye akaunti binafsi huku wakinunua magari.

Mathalani, alisema Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam makadirio yao ni Sh. bilioni 81 mapato yasiyolindwa ni Sh. bilioni 62.2, ikitolewa asilimia 70 ya maendeleo ambayo ni Sh. bilioni 43.587 na kubaki Sh. bilioni 18 kwa ajili ya matumizi mengine kama posho, mafuta.

Halmashauri ya Dodoma makisio ya mapato ni Sh. bilioni 55, mapato yasiyolindwa ni Sh. bilioni 44, inayokwenda kwenye maendeleo ya asilimia 60 ni Sh. bilioni 26, huku matumizi ya kawaida ni Sh. bilioni 17.

Halmashauri ya Kinondoni makisio yao ni Sh. bilioni 57 na yasiyolindwa ni Sh. bilioni 46, matumizi ya maendeleo ni Sh. bilioni 32 na matumizi ya kawaida Sh. bilioni 14.

Alisema Halmashauri ya Arusha makisio ni Sh. Bil. 30, mapato yasiyolindwa Sh. bilioni 24, asilimia 70 ya maendeleo ni Sh. bilioni 17, matumizi ya kawaida ni Shilingi bilioni saba.

"Tumeona mfano mmoja Jiji la Arusha kwa mapato ya Shilingi bilioni saba, wameingiziana fedha kwenye akaunti zao binafsi," alikaririwa.

Gambo alilieleza Bunge kuwa matumizi ya Halmashauri ya Dar es Salaam pekee ni sawa na ya halmashauri ndogo 14 ambazo matumizi ya kawaida kwa mwaka ni Sh. bilioni 9.9, yaani matumizi ya miaka miwili ni ya Halmashauri ya Dar es Salaam, kulipana posho na matumizi mengine.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu alikagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa Mto Sinza/Ng'ombe na Mfereji wa Kiboko katika eneo la Mtogole, akawataka wananchi wa maeneo hayo kutunza mazingira na kuhakikisha hawatupi taka.

Pia aliagiza kufanywa maboresho ya mradi huo kwa kujenga madaraja madogo yatakayowezesha mtu kutoka upande mmoja wa mto kwenda mwingine, pamoja na kuweka taa za barabarani.

Aidha, kiongozi huyo alikagua ujenzi wa soko la wamachinga Mwenge na ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu wa Manispaa ya Kinondoni.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Innocent Bashungwa, alimhakikishia Waziri Mkuu kwamba TAMISEMI kwa kushirikiana na viongozi wa mkoa huo, watatekeleza maagizo hayo.

# Mjadala nauli ATCL kwenda China wamwibua balozi

**Na Jenifer Gilla**

BALOZI wa Tanzania nchini China, Mbelwa Kairuki, ameeleza sababu za kupanda kwa bei ya usafiri wa ndege kwenda nchini China kunatokana na masharti magumu yaliyowekwa na mamalaka za nchini humo dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19 na kupanda kwa bei ya mafuta duniani.

Mwanadiplomasia huyo alitoa ufafanuzi huo baada ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), kutoa taarifa ya kupanda kwa gharama za kusafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Jiji la Guangzough, nchini China.

Kabla ya taarifa ya ATCL, bei hizo zilionekana kusambaa kwenye mitandao ya kijamii na kuzua mjadala kutokana na kupanda kwa gharama hizo.

Shirika hilo lilieleza kuwa linatarajia kurejesha safari za kwenda Guangzhou mara moja kwa wiki China kuanzia Julai 17, mwaka huu, huku nauli kwa daraja la kawaida ikiwa ni Dola za Kimarekani 4,800 (sawa na Sh. 11,191,200.00) na madaraja ya biashara ni Dola 6,850 (Sh. 15,970,775.00).

"Ukweli ni kwamba gharama za usafiri kwenda China kutoka nchi yoyote duniani zimepanda sana. Hali hii imetokana na masharti magumu ya udhibiti wa UVIKO-19 yaliyowekwa na Mamlaka za China," alifafanua.

Alitaja miongoni mwa masharti hayo kuwa ni nchi zinatakiwa kufanya safari moja kwa wiki zikiwa na ujazo usiozidi theluthi mbili ya uwezo wa ndege wa kubeba abiria, lengo likiwa ni kuwapo na umbali kati ya abiria ili kuzuia maambukizi ya UVIKO.

Aliongeza kuwa wakati China ikiweka masharti hayo gharama za uendeshaji zipo pale pale huku kukiwa na ongezeko la bei ya mafuta duniani, gharama zote hizo zitalazimika kubebwa na theluthi mbili ya abiria watakaopanda ndege hizo.

Pia alisema abiria hao pia watalazimika kulipia gharama za ndege kwenda na kurudi kwa sababu ndege hizo zinalazimika kurudi bila abiria, kutokana na masharti yaliyowekwa na mamlaka za nchi hiyo hali inayowazuia watu kutoka nchini humo kwenda nchi nyingine.

Hata hivyo, aliwatoa hofu wananchi kuwa mfumuko huo wa bei ni wa muda mfupi kwa kuwa utakuwa unapungua kadili nchi hiyo itakavyokuwa inalegeza masharti ya udhibiti wa UVIKO -19.

**ATCL NAFUU**

Nipashe ilitembelea ukurasa wa wakala wa tiketi za ndege wa Kayak na kulinganisha bei za usafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Guangzough, kwa wasafiri wa daraja la kawaida na kubaini kuwa unafuu wa gharama hizo kutoka ATCL.

Kwa mujibu wa mtandao huo, gharama za kusafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Guangzough kwa Shirika la Ndege la Ethiopia ni Dola za kimarekani 5,823 (sawa na Sh. milioni 13.57).

Shirika la Ndege la Qatar linatoza Dola za Kimarekani 5,290 (sawa Sh. milioni 12.33), huku gharama za Shirika la Ndege la Emirates likiwa ni Dola za Kimarekani 4,611 (Sh.mil 10.7).

**MJADALA MTANDAONI**

Kufuatia taarifa hiyo baadhi ya Watanzania walilitupia lawama shirika hilo kuwa sio la kizalendo kwa kuwa gharama hizo ni kubwa hasa kwa wafanyabiashara wanaokwenda nchini humo huku wengine wakiona kuwa shirika hilo limetoa gharama nafuu ikilinganishwa na mashirika mengine.

Mwananchi ambaye haridhishwi na gharama hizo alijitambulisha kwa jina la Andiis, aliandika katika ukurasa wa instagram wa shirika hilo kuwa "Nauli ni kubwa sana, mmeangalia vigezo gani mpaka kuweka bei kubwa hivyo ndugu zangu."

Huku mwingine aliyetumia jina la Azees akiandika kuwa "Pamoja ya kuwa inaonekana ni bei ya kushtua, hiyo ni gharama nafuu zaidi kwa safari za kuzidi saa 52 ukilinganisha na mashirika mengine."

HABARI KITAIFA

# ...Mkurugenzi Jiji Dar asimamishwa kazi

**Na Mwandishi Maalum**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amemsimamisha kazi Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Jumanne Shauri na watumishi wengine tisa wa jiji hilo, ili kupisha uchunguzi wa tuhuma za ubadhirifu wa zaidi ya Sh. bilioni 10 zilizokusanywa na hazikuwasilishwa benki kama sheria inavyoelekeza.

Hatua hiyo inatokana na ukaguzi maalum wa mapato ya ndani katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hadi 2020/2021 uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Watumishi hao pia wamekabidhiwa kwa Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Dar es Salaam kwa mahojiano kuhusu tuhuma zinazowakabili.

Uamuzi wa Waziri Mkuu alitangaza jana wakati akizungumza na viongozi wa mkoa wa Dar es Salaam, wabunge, madiwani na watumishi wa Wilaya ya Ilala, katika ziara ya kikazi kukagua miradi ya maendeleo.

Watumishi wengine ni pamoja na Tulusubya Kamalamo (Mweka Hazina), James Bangu (Mhasibu Mapato), Abdallah Mlwale (Mtunza Fedha Mkuu) na Mohammed Khais (Mhasibu wa Masoko).

Alisema watumishi hao walishindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo na hivyo kuisababishia halmashauri hasara ya jumla ya kiasi cha Sh. 10,137,577,401 zilizokusanywa na mawakala na watumishi lakini hazikuingizwa benki.

Wengine ni Jesca Lugonzigwa (Ofisa Hesabu), Josephine Sandewa (Ofisa Hesabu), Tatu Mkangwa (Kibarua) na Felician Maro (Mhasibu Msaidizi) ambao wameisababishia halmashauri hasara ya Sh. 1,214,907,637.

Waziri Mkuu ametaja mawakala wanaodaiwa kufanya udanganyifu wa makusanyo ya mapato kwa kuchezea tarehe za PoS kwa kuzirudisha nyuma na makusanyo ya Sh. 131,356,400 kutoonekana kwenye taarifa za makusanyo ni Pick Trading Ltd na Workers General Supply.

"Ripoti ya CAG imebaini kuwa wataalamu wa halmashauri waliohusika na upotevu wa mapato walikuwa wakiingilia moja kwa moja kati ya mfumo wa LGRCIS na benki na kuandika kwenye mfumo malipo ambayo hayakufika benki kwa lengo la kuficha ukweli wa kasoro na matumizi ya fedha kinyume cha sheria za fedha za umma.

Pia wahasibu waliingiza kwenye mfumo kiasi ambacho hakikupelekwa benki kwa lengo la kupotosha taarifa halisi za makusanyo.

Waziri Mkuu alisema mara kadhaa, Rais Samia Suluhu Hassan alisisitiza umakini kwenye ukusanyaji na matumizi ya mapato, ili kuiwezesha serikali kuendelea kujenga miradi mingi zaidi kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

"Ilala pamoja na kupata hati safi, lakini ndani yake kuna mambo ambayo hayana tija. Uko mwenendo wa kutengeneza udanganyifu katika ukusanyaji na matumizi ya mapato ya halmashauri, kuna wakati wanaamua kuzima kwa saa mbili hadi tatu mfumo kwa kisingizio cha mtandao na mapato yatakayopatikana kwa muda huo hayafuati taratibu kwani badala ya kuipeleka benki inatumika kwa visingizio mbalimbali kama kulipa vibarua," alifafanua.

Ameuagiza uongozi wa halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ufuatilie vyanzo vyote vya mapato vya halmashauri hiyo na pia waweke makadirio ambayo yatawawezesha kukusanya zaidi.

Pia aliwasisitiza kuweke makadirio yatakayowawezesha kufanya kazi zaidi na kila muhusika ahakikishe anatekeleza majukumu yake ipasavyo.

Kikao hicho pia, kilihudhuriwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Innocent Bashungwa, Katibu Mkuu wa TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala na maofisa wengine.

# TIRA yatoa leseni huduma za bima

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Uthibiti wa Bima Tanzania (TIRA), imetoa leseni ya huduma kwa kampuni tatu nchini, kwa ajili ya kutoa huduma hiyo kwa njia ya mtandao.

Akizungumza kwenye viwanja vya Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Mwalimu Julius Nyerere (DITF), Kamishna wa Bima kutoka Mamlaka hiyo, Baghayo Saqware, alisema leseni hizo zimetolewa kwa kampuni hayo baada ya kufikia vigezo na hatua hiyo itawasaidia wananchi kupata huduma za bima wakati wowote kupitia mitandaoni.

Alisema leseni hizo zimetolewa baada ya kufuata utaratibu na kampuni zilizopewa kufikia vigezo vinavyotakiwa.

"Vigezo vilivyowekwa ili kampuni kupata leseni ni pamoja na mtaji usiopungua Sh. milioni 100 kwa ajili ya wateja wanaoweza kupata matatizo fedha hizo zikafidia, vigezo vingine ni kampuni husika kuwa na wataalamu wa masuala ya mtandao ambao wataweza kuendesha teknolojia hiyo," alisema Saqware.

Alisema TIRA ilikuja na huduma hiyo ya uthibiti wa bima kwa njia ya mtandao (IDF) baada ya kupitishwa rasmi Mei, mwaka huu na itakuwa ikihakikiwa baada ya miaka mitatu.

Alisema huduma hiyo pia itawasaidia wananchi kupata huduma wakiwa sehemu yoyote bila kulazimika kufika kwenye ofisi za bima.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa M-Pesa kutoka kampuni ya Vodacom, Epimack Mbeteni, alisema kupewa leseni hiyo ni hatua kubwa kwa kampuni yao katika kufikia malengo ya kuhudumia wateja wao.

"Kampuni yetu ina wateja wa M- Pesa zaidi ya milioni 10 nchi nzima, leseni hii tuliyopewa itasaidia kufikisha huduma ya bima katika kiwango cha juu," alisema.

Aidha, TIRA ilisema imeshaunganisha kampuni 12 za bima kutoa huduma hiyo kwa wateja wake.


# NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD**, kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| KIJITONYAMA | MAMII BUSINESS CENTRE | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NAMBA 83 KITALU 'A' NA HATI NAMBA 46339 | MARY JAMES MNYUNE | BOKO-KINONDONI | 26/07/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MAIN | CHEX ENGINEERING LTD | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NAMBA 110 KITALU '15' NA HATI NAMBA 69065 | CHEDIEL GASPER NSHANA | BUNJU-KINONDONI | 26/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ARNOLD CONRAD MTENGA | NYUMBA | ARNOLD CONRAD MTENGA | SALASALA- KINONDONI | 26/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | NEEMA STANLEY MOTELWA | NYUMBA | MOHAMED ALLY VUYAA | RADA MOJOHE-ILALA | 27/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | IBRAHIMU ELIUD MANOSHI | NYUMBA | IBRAHIMU ELIUD MANOSHI | VIKAWE KIBAHA- PWANI | 28/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | SHUKURANI JOSEPHAT MHAWI | NYUMBA | MOHAMED RAMADHANI | NDUBWI MBEZI JUU- KINONDONI | 28/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | BARAKA NELSON NYIRENDA | PAGALE | BARAKA NELSON NYIRENDA | BUNJU 'B' | 27/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | MBALIZI SUPER SEMBE | NYUMBA | ELIAS JOSEPH MWANTANJI | BOKO -KINONDONI | 27/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | MBOPO HARDWARE AND TOFALI INVESTMENT | NYUMBA | MBOPO HARDWARE AND TOFALI INVESTMENT | MBOPO MABWEPANDE- KINONDONI | 28/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ROSE JOHN KUNDY | NYUMBA | ROSE JOHN KUNDY | UDINDIVU MAPINGA BAGAMOYO-PWANI | 27/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | AMA ABDALLAH KIPENDE | NYUMBA | AMA ABDALLAH KIPENDE | KIBAONI KISARAWE - PWANI | 27/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | MDAKI NASSORO KABELELE | NYUMBA | MDAKI NASSORO KABELELE | VIWEGE MAJOHE | 28/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | EPAFRASI FIDELIS JULIUS | NYUMBA | EPAFRASI FIDELIS JULIUS | MONGALANDEGE | 28/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | WARIOBA WILSON MAHATANI | NYUMBA | WARIOBA WILSON MAHATANI | MBONDOLE | 27/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | RITHA MARTIN LUABUGANDA | NYUMBA | RITHA MARTIN LUABUGANDA | KIGAMBONI | 26/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | SHAMSI FADHILI MASISA | NYUMBA | SAAD ADAM MDOE | KINYAMWEZI KATA YA PUGU | 27/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | YVONNE MAJEVU KUMBI | NYUMBA | AYUBU AUGUSTINO MSULE | KIBAMBA-UBUNGO | 28/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | MWANAHAMIS VITUS FRANK | NYUMBA | HADIJA MOHAMED CHANDE | MSINGWA-MSIGANI | 28/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | SELEMANI HEMED SELEMANI | NYUMBA | SELEMANI HEMED SELEMANI | MBAGALA KIBONDE MAJI | 29/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | ABDI SAID SELEMANI | NYUMBA | ALLY MOHAMED LIKOMELA | MBAGALA RANGI TATU | 29/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | PADONI KIBAYU SIMON | PAGALE | PADONI KIBAYU SIMON | VIWEGE-MAJOHE | 28/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | RAHABU ERASTO MESSO | NYUMBA | RAHABU ERASTO MESSO | KWEMBE-UBUNGO | 28/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | MICHAEL HAYSHI QAMARA | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NAMBA 53 KITALU 'C' NA HATI NAMBA 35227 | MICHAEL HAYSHI QAMARA | KARATU | 27/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

218939901

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14

2 Ikiwamnunuziatashindwakutimizashartilolote la mnada kuhusiana na malipo yaawali,hatarudishiwapesayoyotealiyokwishailipa

3 Kwa mawasiliano zaidi; **tupigie simu no.0714939933/0718038313/0785242219/0765999000**

4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

HABARI KITAIFA

# 22 kizimbani wakikabiliwa shtaka la wizi wa mamilioni

Na Grace Gurisha

WAKAZI 22 wa Jiji la Dar es Salaam wamefikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakikabiliwa na mashtaka nane likiwamo la wizi wa Sh. milioni 780.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ester Martin akisaidiana na Wakili wa Serikali, Timotheo Mmari, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Ramadhani Rugemalira kuwa Menjestu Mselema (44) na wenzake 22 wanatuhumiwa kwa makosa nane.

Washtakiwa wengine ni Tulipo Mwakuzi (40), Bernard Machimbo, Joseph Mwatonoka, Juma Mbulinda, Joseph Mpondo maarufu kama Khomango, Jabiri Mgoli, Englibert Masare, Beda Mmali, Kaisi Nasibu, Bernadetha Mwakuzi na Godwin Erio, wote wakazi wa Jiji la Dar es Salaam.

Wengine ni Anold Erio, Agnes's Mselema, Florah Mwita, Oswald Mselema, Olaph Mselema, Janeth Shilla, John Mkamba, Edes Hyera, Sylidion Odilo, Said Mkimu na Grace Komba.

Mmari alidai katika shtaka la kwanza, washtakiwa kwa pamoja wanadaiwa katika kati ya Juni mosi, 2020 na Juni 8, 2020 katika Jiji la Dar es Salaam walikula njama za kutenda kosa la wizi.

Shtaka la pili ni wizi na linawahusu washtakiwa wote, ambao wanadaiwa Juni 8, 2020, katika Benki ya NMB tawi la Mbezi Beach, walijipatia Sh. milioni 780 mali ya Kampuni ya SGA.

Shtaka la tatu la utakatishaji fedha, linalowakabili washtakiwa 20, isipokuwa mshtakiwa Odilo, Mkimu na Komba, wanadaiwa Juni 8, 2020 na Agosti 31, 2020 katika Jiji la Dar es Salaam, walijipatia Sh. milioni 780 wakati wakijua fedha hizo ni zao la kosa la wizi.

Shtaka la nne ni kutakatisha fedha linalomkabili mshtakiwa Mwakuzi, ambaye anadaiwa kutenda kosa hilo Julai mosi 2018 na Mei 30, 2020 katika maeneo tofauti ya Makambako, mkoani Njombe.

Mwakuzi anadaiwa siku hiyo, kwa lengo la kuficha uhalali wa fedha, alitumia sehemu ya Sh. milioni 780 kununua pikipiki moja, wakati akijua fedha hizo ni kosa tangulizi la wizi.

Pia siku na eneo hilo, Mwakuzi kwa lengo la kuficha uhalali wa fedha anazodaiwa kuiba, alitumia sehemu ya Sh. milioni 780 kununua Power tiller, wakati akijua fedha hizo ni kosa tangulizi la wizi.

Katika shtaka la kutakatisha fedha, linalomkabili Joseph Mwatonoka, anadaiwa Mei 20, 2020 katika maeneo ya Chimala mkoani Mbeya, kwa lengo la kuficha uhalali wa fedha, mshtakiwa alitumia sehemu ya Sh. milioni 780 kwa kununua magunia 910 ya mpunga yenye thamani ya Sh. milioni 47.2 wakati akijua fedha hizo zinatokana na kosa tangulizi la wizi.

Baada ya kusomewa mashtaka yao, Wakili Martin aliieleza Mahakama hiyo kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka amewasilisha hati ya kuruhusu Mahakama hiyo kusikiliza shauri hilo.

Upande wa mashtaka ulidia kuwa upelelezi wa shauri hilo umekamilika, wanaomba kupangiwa tarehe nyingine kwa ajili ya kuwasomea hoja za awali.

Hakimu Rugemalira, aliahirisha kesi hiyo hadi Julai 21, 2022 kwa ajili ya kusomewa hoja za awali.



Jenise Mpanju (kushoto) ambaye ni mwanafunzi wa mwaka wa pili wa Shahada ya Ustawi wa Jamii katika Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU), akimpima shinikizo la damu mmoja wa watu waliofika kwenye kambi ya kupima afya bure inayoendelea kwa mwezi mzima viwanja vya Mlimani City jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Maofisa maendeleo wapewa pikipiki Kahama

Na Shaban Njia, KAHAMA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, imekabidhi pikipiki 19 zenye thamani ya Sh. milioni 57.9 kwa maofisa wa maendeleo ya jamii ngazi ya kata, ili kusimamia vyema miradi ya maendeleo ya wananchi na vikundi vya wajasiriamali.

Fedha za ununuzi wa pikipiki hizo zinatokana na mapato ya ndani ya halmashauri ya bajeti iliyotengwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, kwa ajili ya kuwarahisishia utendaji kazi watumishi ngazi ya kata.

Akikabidhi pikipiki hizo jana, Mwenyekiti wa Manispaa hiyo, Yahaya Bundala, aliwataka kuzitumia kwa kazi husika na atakayebainika kutumia kinyume cha matumizi atawajibishwa kisheria na kunyang'anywa.

Pia aliwataka kusimamia vyema miradi ya maendeleo kwenye kata zao ili manispaa hiyo iweze kusonga mbele kitaifa kwa kufanya vizuri.

"Leo hii tunawakabidhi pikipiki hizi ili ziwe msaada kwenu kusimamia miradi yetu ya maendeleo, tunawaomba mhakikishe mnazitunza na kukaa nazo muda wote wa kazi na sio mnatoka hapa na kuwakabidhi watu waziendesha na kuanza kufanya biashara," alionya Bundala.

Awali, akitoa taarifa ya ununuzi wa pikipiki hizo, Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Clemensi Mkusa, kwa niaba ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, Anderson Msumba, alisema fedha za ununuzi zinatokana na mapato ya ndani kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022.

Alitaja mgawanyo wake kwa kila idara na idadi kwenye mabano kuwa ni Kilimo (9), Maendeleo ya Jamii (5), na Utawala (5).

Mmoja wa wanufaika, Ofisa Kilimo wa Kata ya Kilago, Costantine Bruno, alisema awali walilazimika kutembea umbali wa kilomita nane hadi 12 kwa siku kuwafuata wananchi na kuwapatia huduma na kuahidi kwa usafiri huo watawafikia wengi na kuwahudumia vyema.

Alisema pia wanaiomba manispaa kuona umuhimu wa kuwapa fungu la mafuta ya kutumia kila mwezi hasa nyakati za majira ya masika, ili kufika katika maeneo ya kilimo kwa haraka kwa kuwa vijiji vingi vipo pembezoni mwa mji.

Naye Ofisa Mtendaji wa Kata wa Busoka, alisema pikipiki hizo zitasaidia kuzungukia vikundi mbalimbali vya ujasiriamali katika kata zao na kuhakikisha mikopo ya halmashauri inarejeshwa kwa wakati.

# Magari 1,000 yafungwa mfumo wa gesi

Na Grace Gurisha

KAMPUNI tanzu ya Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam (DIT Ltd), imesema mfumo wa kuongeza gesi kwenye magari umefikia zaidi ya magari 1,000, lengo ni kupunguza gharama za mafuta.

Hayo yamesemwa jana na Mkuu wa Kitengo cha Mauzo katika kampuni hiyo, Agnes Kimwaga, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika maonyesho ya 46 ya Biashara (DITF) Sabasaba, jijini Da es Salaam.

Alisema mfumo huo wa petroli utaendelea kuwapo kama kawaida wanachoongeza ni wa gesi ambao unasaidia kupunguza gharama za mafuta kwa kiasi kikubwa kwa kufunga mitungi ya kilo tofauti.

Vile vile, alisema kilo moja ya gesi kwenye magari ambayo hayana matumizi makubwa ya mafuta, ni Sh. 1,550 kwa kilometa 20.

Kuhusu muda wa kuweka mfumo, alisema kama hakuna foleni ni siku moja mteja anarudishiwa gari yake. Aidha, alisema gharama silinda nne ni Shilingi milioni mbili, silinda sita Sh. milioni 2.5 na silinda nane Sh. milioni 2.8.

Kwa mujibu wa Kimwaga, wapo kwa ajili ya kutatua changamoto za jamii na sio kufanya biashara, hasa wakati huu ambao gharama ya mafuta zipo juu, na mfumo huo utapunguza gharama kwa kiasi kikubwa.

"Kama kila siku ulikuwa unatumia Sh. 30,000 utajikuta unatumia Sh. 15,000. Kuna wanafunzi wanatengeneza viti ambavyo vinaweza kutumiwa na wenye ulemavu jukumu letu ni kuzitangaza na kupeleka sokoni kupata wanunuzi," alisema Kimwanga. Alisema DIT itaendelea kuboresha na kuuza bunifu mbalimbali zilizobuniwa na wanafunzi pamoja na wakufunzi kwa gharama nafuu, ili kutatua changamoto mbalimbali kwenye jamii.

"Tunazalisha bidhaa nyingi ambazo zilikuwa zinakaa makabatini na kujaa vumbi hivyo tukaona ni bora bunifu hizi tuziboreshe zaidi na kuziingiza sokoni. Kwa hiyo tumekuja na mashine mbili mojawapo inayowezesha kubangua karanga na inayochakata plastiki na kutengeneza vipuri vya bajaji," alisema Kimwaga.

Kadhalika, vipuri hivyo pamoja na mashine ya kubangua karanga vinauzwa kwa bei ya jumla na rejareja huku gharama zake zikiwa chini tofauti na bidhaa zinazoingizwa kutoka nje lengo ni kuwawezesha Watanzania wote kupata bidhaa hizo kwa gharama nafuu.

"Tumepata wateja wengi hapa Sabasaba kwa sababu gharama zetu ziko chini kuliko vilivyopo kwenye soko la kawaida na hii tunataka wamiliki na madereva wa bajaji wengi wasitafute vipuri feki wapate hizi za kwetu ambazo gharama zake ni nafuu na bora," alisisitiza.

Alisema kampuni hiyo imefanikiwa kufanya kazi mbalimbali ikiwamo za ujenzi, maabara na uwekaji wa taa za kuongozea magari mikoa ya Kanda ya Ziwa na Dar es Salaam.

Pia wameshiriki kwenye uwekaji wa majina ya mitaa pamoja na programu ya daktari kumhudumia mgonjwa bila kuonana ana kwa ana.

HABARI KITAIFA

# TMA yahakikishiwa uwekezaji miundombinu ya utabiri

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema itaendelea kuwekeza katika miundombinu ya Hali ya Hewa nchini ili kuongeza usahihi wa utoaji wa taarifa kwa wadau wote wakiwamo usafiri wa anga, ulinzi, uvuvi na usafiri wa nchi kavu.

Akizungumza baada ya kutembelea rada ya hewa iliyojengwa mkoani Mtwara, Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete, alisema uhakika wa utabiri utachangia umakini katika uendelezaji wa miundombinu nchini katika nyanja zote.

"Nawapongeza sana kwa kukamilisha mradi huu na nichukue fursa hii kuwaambia wananchi kuwa serikali tayari iko kwenye hatua mbalimbali za kuongeza rada kufikia saba ili kuhakikisha usahihi wa utabiri unaongezeka," amesema Naibu Waziri Mwakibete.

Naibu Waziri Mwakibete alisema pamoja na uwezekezaji huo amewataka Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini (TMA) kuhakikisha inabuni njia mbalimbali za kutoa taarifa ili kuwafikia wadau wote kwa wakati na kurahisisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Naye Mbunge wa Mtwara Mjini, Hassan Mtenga, ameiomba wizara kuijenga barabara inayoingia kwenye miundombinu kwa kiwango cha lami kwa kuwa inapata changamoto hasa nyakati za mvua.

"Wizara hii ina fedha hebu tizama kwenye bajeti angalau kilomita hizi chache mziwekee lami ili kulinda miundombinu hii mliyoijenga kwa fedha nyingi," alisisitiza Mbunge Mtenga.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Miundombinu wa TMA, Dk. Paschal Waniha, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuwekeza katika miundombinu ya hali ya hewa na kuwa uwapo wa rada hizo umeanza kuleta mabadiliko hasa kwa wadau wa mikoa ya kusini.

Kuhusu utabiri kuwafikia wadau, Dk. Waniha alisema TMA inatumia njia za ujumbe mfupi (sms), mitandao ya kijamii, maonyesho mbalimbali ya kitaifa na kutumia vyombo mbalimbali vya habari lengo likiwa kuwafikishia taarifa sahihi na kwa wakati.

Naibu Waziri Mwakibete yuko mkoani Mtwara kwa ziara ya siku tatu kukagua miundombinu inayojengwa na wizara mkoani humo.

**Naye Mbunge wa Mtwara Mjini, Hassan Mtenga, ameiomba wizara kuijenga barabara inayoingia kwenye miundombinu kwa kiwango cha lami kwa kuwa inapata changamoto hasa nyakati za mvua.**

# UNFPA yaona ongezeko la watu, ukatili kijinsia

**Na Martha Magawa**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA), limesema kuwa miezi michache ijayo kutakuwa na watu bilioni nane ulimwenguni, huku kukiwa na ongezeko la ukatili wa kijinsia.

Aidha, limesema ni muhimu watu wakahakikisha wanatimiza Malengo Endelevu ya Milenia kuelekea mwaka 2030 kwa kuhakikisha wanatokomeza vifo vya mama na mtoto, ukatili wa kijinsia na mila kandamizi.

Katika taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Mkurugenzi Mtendaji wa UNFPA, Dk. Natalia Kanem, kuhusu maadhimisho ya siku ya idadi ya watu duniani, aliwataka wananchi kukumbuka kuwa ongezeko hilo ni hatua itakayowavutia watu wengi. Dk. Kanem alisema ongezeko hilo litaendelea kuwa mjadala duniani kwa kuwa ni maendeleo ya binadamu katika nyanja za kiafya, uchumi, elimu na ukuaji wa sayansi na teknolojia.

Aidha, Mkuu wa Mawasiliano kutoka UNFPA, Warren Bright, alisema kaulimbiu ya mwaka huu ni 'dunia ya watu bilioni nane', na nchini kitaifa yatafanyika wilayani Hanang mkoani Manyara kuanzia Julai 17, mwaka huu, ambako pamoja na mambo mengine kutakuwa na mdahalo wa vijana kuhusu ukatili wa kijinsia.

Alisema siku ya kilele ni Julai 20, mwaka huu na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Katika hatua nyingine, UNFPA imewataka Watanzania kujitokeza kwa wingi kushiriki sensa ya watu na makazi itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu, ili kupatikana kwa takwimu sahihi kwa maendeleo ya taifa.

"Hakuna Shirika la Idadi ya Watu Duniani bila sensa, hivyo sisi kama wadau wakubwa wa maendeleo ya watu tunasisitiza watu kuhesabiwa na kutoa taarifa sahihi, ili kila mmoja asiachwe nyuma katika kupanga maendeleo ya taifa na kufikiwa na huduma bora za afya na elimu," alisisitiza Warren.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (kushoto), akiwa na ujumbe wa Benki ya Dunia ukiongozwa na Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia, anayesimamia Kanda ya Kusini Mashariki mwa Afrika, Victoria Kwakwa (kulia), katika kikao kilichofanyika ofisi ndogo za Wizara ya Fedha na Mipango, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uhusiano Tanzania, Benki ya Dunia waimarika

**Na Benny Mwaipaja**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba amesema kuwa uhusiano kati ya serikali na Benki ya Dunia unazidi kuimarika na Watanzania watarajie maendeleo makubwa kupitia ushirikiano huo.

Dk. Nchemba alisema hayo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), jijini Dar es Salaam baada ya kumpokea Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia anayesimamia Kanda ya Kusini mwa Afrika, Victoria Kwakwa, aliyewasili nchini kwa ziara ya kikazi ya siku mbili kwa mwaliko wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Aliishukuru Benki ya Dunia kwa kuisaidia nchi kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika nyanja mbalimbali za kijamii na kiuchumi ikiwamo ujenzi wa miundombinu, elimu, afya, mazingira na kupitia mpango wa mikopo nafuu wa dirisha la IDA 19 ambao umemaliza muda wake na pia nchi inatarajia kupata fedha nyingine za kutekeleza miradi ya maendeleo kupitia dirisha jipya la IDA 20.

Kwa upande wake, Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia anayesimamia Kanda ya Kusini Mashariki mwa Afrika, alisema kuwa lengo la ziara yake nchini Tanzania ni kujitambulisha na kuimarisha ushirikiano kati ya Tanzania na Benki hiyo baada ya kuchukua nafasi ya aliyekuwa Makamu wa Rais wa Benki hiyo Kanda ya Kusini Mashariki mwa Afrika, Dk. Hafez Ghanem, ambaye amestaafu.

Akiwa nchini, Kwakwa, anatarajiwa kukutana na kufanya mazungumzo na Rais Samia, Ikulu Dar es Salaam, baadaye ataelekea Visiwani Zanzibar na kukutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, na atakutana pia na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Nchemba na viongozi wengine wa serikali.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ziara ya Makamba mikoani iongeze kasi upatikanaji umeme

**JUZI**, Waziri wa Nishati, January Makamba, alieleza mpango mkakati wa wizara hiyo wa siku 21 wa kuanza ziara ya kutembelea mikoa 14 na wilaya 38, hususani maeneo ya vijijini.

Lengo la ziara hiyo ni kukagua na kusimamia miradi inayotekelezwa na wizara na taasisi zake, kuzungumza na wananchi na kupokea kero, maoni, ushauri na kutoa majawabu na ufumbuzi na ufafanuzi wa masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya nishati.

Aliitaja mikoa atakayofikiwa na huduma hiyo ni Mara, Mwanza, Geita, Simiyu, Kagera, Shinyanga, Tabora, Katavi, Rukwa, Sogwe, Mbeya, Njombe, Ruvuma na Mtwara.

Maeneo yatakayopewa kipaumbele ni upatikanaji na matumizi ya nishati safi na salama ya kupikia, usambazaji wa umeme vijijini na vitongoji, upatikanaji wa umeme wa uhakika.

Pia uboreshaji wa huduma zinazotolewa na taasisi za wizara, usambazaji wa mafuta salama na ya bei nafuu vijijini.

Tunaamini kupitia ziara hiyo Watanzania wengi wanaoishi maeneo ya vijijini wanakwenda kupata umeme ipasavyo, kuanzia walioomba kuunganishiwa na kulipa na wanaotamani kufikiwa na huduma hiyo.

Tunafahamu juhudi za serikali za kutaka kuwafikishia umeme wananchi wa vijijini kwa wakati kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (REA), lakini baadhi ya makandarasi wamekuwa kikwazo kwa miradi hiyo.

Ili kuondokana na kero ya makandarasi katika kusambaza umeme, ni muhimu nchi ikajipanga vyema kwenye kuendeleza vyanzo vya nishati jadidifu kwa kuwa ndiyo msukumo wa dunia, lakini kuendelea kushirikiana na sekta binafsi ili huduma iwafikie wananchi wengine na kwa haraka.

Wakati tukiendelea na vyanzo vilivyozoeleka ni muhimu kuwekeza na kuwa makini na uwekezaji unaofanywa kwenye vyanzo vya nishati jadidifu ambavyo ni rafiki kwa mazingira ambavyo ni jua, upepo, mawimbi na upepo wa bahari na tungamotaka, ili inapofika ulazima wa kuachana na gesi, mafuta na maji kuwe na maandalizi ya kutosha.

Maji ni chanzo kizuri cha kuzalisha umeme, lakini kutokana na mabadiliko ya tabianchi inapotokea ukame vyanzo hukauka na kushindwa kuzalisha nishati hiyo, mara kadhaa Tanzania imepitia mgawo sababu ikiwa ni kukauka kwa mabwawa ya kuzalisha nishati hiyo.

Hivyo, tunaamini kuwa ziara ya Waziri Makamba inakwenda kumaliza kabisa ama kupunguza tatizo la kukatika umeme ovyo nchini.

Watanzania wanaimani na serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, sio vyema kumwangusha kwa kuwapo kwa tatizo la kukatika kwa umeme, ni muhimu kuona uhalisia kwamba umeme haukatiki na kama ikitokea umekatika wananchi waelezwe tatizo.

Tunaamini ziara ya Waziri Makamba inakwenda kuzaa matunda ya kutokomeza tatizo hilo, kwa sababu limekuwapo kila mwaka hasa wakati wa ukame kwa sababu siku 21 si haba.

Kwenye ziara hiyo, imetajwa mikoa mingi ikiwamo Songwe na Mbeya, ni wakati mwafaka kwa Waziri Makamba kwenda kuangalia chanzo cha nishati jadidifu (umeme wa joto ardhi) ambalo lipo kwa wingi mikoa ya Songwe, Mbeya na kwingine.

Majirani zetu Kenya wanazalisha umeme wa joto ardhi kwenye bonde la ufa ambalo limepita pia Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara nchini ambako kuna majimoto ambalo halijatumiwa vyema.

Kwa mujibu wa Wikipedia, inakadiriwa Bonde la Ufa lina uwezo wa kuzalisha megawati 2,000 iligundulika mwaka 1956 eneo la Olkariana uzalishaji ulianza mwaka 1981 zilizalishwa megawati 15 na sasa wanazalisha MW 256 na wanatarajia kufikia 576 ndani ya miaka 20 ijayo.

Jitihada ni kubwa na sasa utafiti umeshafanyika, lakini kasi iongezeke ili nchi iwe na vyanzo tofauti tofauti vya umeme kuondokana na kutegemea umeme wa maji pekee, ambao haijaonyesha mafanikio kwa miaka mingi hasa kipindi hiki cha mabadiliko ya tabia nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ajira za walimu ziguse uwiano wa shule za mijini na vijijini

Na Sabato Kasika

**SERIKALI** imeajiri walimu 9,800, ambao sasa wanatakiwa kuripoti kwenye vituo vipya vya kazi ili waanze kutekeleza majukumu yao ya kufunza na kufundisha watoto katika shule za msingi na sekondari.

Ajira mpya huenda zikasaidia kupunguza changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikiwakumba walimu, wanafunzi na hata wazazi na walezi, huku chanzo chake kikidaiwa kuwa ni uhaba wa walimu.

Miongoni mwa changamoto hizo ni baadhi ya shule kuwa na walimu wachache ambao hulazimika kufundisha vipindi vingi, huku wanafunzi nao wakikosa baadhi ya masomo kutokana na uhaba huo.

Uhaba huo pia umekuwa ukisababisha wazazi na walezi kubebeshwa mzigo kwa kutozwa fedha za masomo ya ziada 'twisheni', kwani wakiwa shuleni, hawasomi vipindi vyote kutokana na uhaba huo.

Hivyo, hatua ya kuajiriwa kwa walimu wapya 9,800 kunaweza angalau kupunguza baadhi ya changamoto ambazo zinasababishwa na uhaba huo, hasa shule za vijijini ambazo zina walimu wachache zaidi.

Serikali inawataka waajiriwa hao wapya kuripoti kwa wakurugenzi wa halmashauri walizopangiwa wakiwa na kitambulisho cha taifa au namba ya utambulisho ya NIDA, cheti halisi cha kuzaliwa, ni vyema wafanye hivyo.

Ninaamini kuwa hatua ya serikali kuajiri walimu, inalenga kupunguza changamoto ambayo imekuwapo kwenye baadhi ya shule, ikiwamo ya kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi huku walimu wakiwa wachache.

Pamoja na hayo, ninadhani suala la uhaba wa walimu lingefaa kufanyiwa kazi kwa njia ya hii pia, ya kuwa na uwiano kati ya walimu wa shule za mijini na vijijini, badala ya upande mmoja kuwa na mrundikano wa walimu.

Pamoja na hayo, ninadhani suala la uhaba wa walimu lingefaa kufanyiwa kazi kwa njia ya hii pia, ya kuwa na uwiano kati ya walimu wa shule za mijini na vijijini, badala ya upande mmoja kuwa na mrundikano wa walimu.

Mfano, Desemba 2016, takwimu za Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) zilieleza kuwa kulikuwa na walimu 272,264 wa shule za msingi na sekondari kutoka 153,767 mwaka 2005.

Lakini, ikabainika kuwa shule nyingi za vijijini zina uhaba mkubwa wa walimu, tofauti za mijini ambazo walimu wamerundikana, hivyo ingefaa suala la uwiano kati ya shule za mijini na vijijini likatiliwa mkazo.

Nakumbuka mwaka jana, aliyekuwa Waziri wa TAMISEMI, Ummy Mwalimu, alitangaza kuwa, walimu wanaotaka kuhama kutoka mijini kwenda vijijini ruksa, na akaweka masharti kwa wanaohamishwa vijijini kwenda mjini.

Kwamba, walimu wanaotaka kuhama kutoka vijijini kwenda mjini, lazima Tume ya Utumishi wa Walimu nchini, ihakikishe kabla ya kuwahamishwa wawe na walimu mbadala wa kule wanakotoka.

Lengo lake lilikuwa ni kukabili uhaba wa walimu katika shule za vijijini, hivyo kwa mtazamo wangu, ninadhani pamoja na kuajiri walimu wapya, bado ipo ya kudhibiti wingi wa walimu kwenye shule za mijini.

Kama alivyowahi kusema Waziri Ummy, kuwa ni uhamisho ni haki ya mtumishi, lakini ni vyema akawapo mwingine wa kuziba nafasi ya anayehama, vinginevyo shule za vijijini zitaendelea kuwa na uhaba wa walimu.

Lakini, ingekuwa vyema kama Tume ya Utumishi wa Walimu itafanya tathmini ya kina kwa kuangalia uwiano wa walimu kwenye shule za msingi na sekondari katika mamlaka za serikali za mitaa.

Hatua hiyo iwe ni kwa ajili ya takwimu sahihi za mahitaji halisi ya walimu na uwiano uliosawa katika halmashauri badala ya upande mmoja kuwa na mrundikano huku shule nyingine zikiwa na uhaba mkubwa wa walimu.

Pamoja na hayo, jambo lingine ambalo ninadhani linaweza likasaidia kupunguza walimu kuhama kutoka shule za vijijini, ni kuboresha mazingira ya huko ikiwamo nyumba kuwa mahata usafiri ili wafike kazini kwa wakati.

Kumekuwapo na malalamiko kuwa mazingira duni ya shule za vijijini ni kikwazo kwa walimu, na inawezekana yanachangia hata baadhi yao kuandika sababu za uongo, ili mradi wahamishwe kutoka katika mazingira hayo.

Lakini, mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji, katika shule za vijijini, ni vyema yakawa rafiki kwa walimu na wanafunzi, hatua ambayo ninadhani inaweza kupunguza kasi ya walimu kukimbilia shule za mijini.

Ikumbukwe kuwa bila kuboresha mazingira ya shule za vijijini, ufundishaji na ujifunzaji unaweza kuendelea kuwa mgumu na hivyo kuwafanya wanafunzi kushuka kitaaluma au kufaulu kwa alama ndogo.

# Wakulima washauriwa kupeleka ufuta ghalani

**Na Julieth Mkireri,** RUFIJI

MENEJA wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkoa wa Pwani (CORECU), Mantawela Hamis, amewashauri wakulima wa ufuta ambao hawajapeleka mazao yao kwenye maghala wasisubiri kupanda kwa bei.

Alitoa ushauri huo juzi kwenye mnada wa ufuta uliofanyika katika Wilaya ya Rufiji huku kilo moja ikiuzwa kwa Sh. 3,090 .02 kutoka Sh. 288 ya mnada wa kwanza.

Alisema kitendo cha kuendelea kukaa na ufuta nyumbani kinaweza kuwasababishia hasara kutokana na bei kushuka na kutokuwapo kwa minada hali itakayowafanya wapate hasara.

"Bei za ufuta zimeendelea kupanda na leo katika mnada huu wa sita tumeuza kilo moja kwa Sh. 3,090.02, sasa kuna wale wakulima bado hawajaleta ufuta wao kwenye vyama vya ushirika, rai yangu kwao wahakikishe wanatumia muda huu kupeleka ufuta wao ili wasije wakapata hasara maana bei zinaweza zikashuka tofauti na walivyotegemea," alisisitiza.

Meneja huyo alisema kikwazo kipo kwenye fedha kuwafikia kwa wakati wakulima baada ya kuuza ufuta wao ambacho aliahidi kuwa kinafanyiwa kazi kuondoa lawama wanazokutana nazo viongozi wa Amcos na CORECU.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa CORECU, Musa Mng'elesa, aliwataka wakulima wa korosho kuanza kutumia sulpher za maji kutokana na kikwazo cha upatikanaji wa unga.

Alisema mwaka huu walihitaji kupata pembejeo tani 1,600 na mpaka sasa wamepokea 205 na kwa upande wa sulpher za unga wanatarajia kupata nusu tofauti na mahitaji.

Aliwataka viongozi wa AMCOS kutoa ushauri kipaumbele wapewe wakulima wazalishaji wa korosho na hali ya uzalishaji.

Mng'elesa alisema kwa sasa zaidi ya tani 600 za sulpher na lita 100,000 za viuatilifu vya maji vimepokelewa na chama hicho na vinasambazwa kwa gharama za CORECU baada ya kupokelewa kutoka serikalini.

Aliziomba halmashauri za mkoa huo kutumia ushuru wanaopata kurudisha kwa wakulima kwa kununua pembejeo ili ziweze kutosheleza kwa mahitaji ya wakulima na kukuza uzalishaji.

Mwenyekiti alisema uzalishaji wa ufuta kwa mwaka huu umekua baada ya chama hicho kusambaza tani 10 za mbegu ya ufuta pamoja na boksi 500 za viuatilifu.

Baadhi ya wakulima wa ufuta waliiomba CORECU kusimamia upatikanaji wa fedha zao kwa wakati baada ya kuuza zao lao kwenye minada ambayo imefanyika katika mkoa huo.

# Wanaobeza mradi bomba la mafuta TZ-Uganda wamkera Katibu Mkuu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Nishati, Felchesmi Mramba, amesikitishwa na baadhi ya wanaharakati wa mazingira nchini Uganda, wanaobeza mradi wa bomba la mafuta, kwenye mitandao ya kijamii wakidai utaharibu mazingira.

Alisema kabla ya utekelezaji wa mradi huo, serikali za pande zote mbili zilikubaliana kutumia mafuta hayo kuzalisha nishati ya umeme katika chanzo cha mafuta na vituo 14 vya kuchemsha mafuta hayo, lakini baadaye walibadilisha ilipoonekana watachafua mazingira kwa hewa ukaa.

Mramba aliyabainisha hayo jana mkoani Tabora wakati wa ziara ya siku moja ya kukagua ujenzi wa kiwanda cha kuweka plastiki kwenye mabomba yatakayopitisha mafuta kutoka nchini Uganda hadi Chongoleani mkoani Tanga, kinachojengwa Kata ya Igusole Sojo, wilayani Nzenga.

Alisema mazingira yamepewa kipaumbele katika utekelezaji wa mradi huo na watatumia mafuta kuzalisha nishati ya umeme.

Aidha, baada ya kufanya tathmini upya ya utunzaji wa mazingira walikubaliana kutumia nishati ya umeme, na Uganda wamesafirisha umeme kutoka mtambo wa maji wa Karuma hadi kwenye mitambo ya mradi huo.

Kwa upande wa Tanzania, alisema mafuta hayo hayatatumika kama walivyokubaliana awali na badala yake watatumia umeme wa jua (sola) na TANESCO, katika vituo vyote 14, mahitaji ni megawati 25 ambazo zitachemshia mafuta hayo.

"Tukitumia mafuta haya kwa ajili kuzalisha nishati italeta hewa ukaa na kuharibu mazingira na ndiyo maana tutatunza mazingira yetu kwa kutumia umeme wa jua na TANESCO," alisisitiza Mhandisi Mramba.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba alisema, mradi huo utakapokamilika utagharimu Sh. trilioni 11.8, kati hizo Sh. bilioni 260 zimeshatolewa.

Alisema mradi utakapokamilika serikali itapata manufaa makubwa na kuwataka wananchi wanaoishi jirani na bomba hilo kutunza miundombinu huku akiainisha ajira za sasa zitakuwa 10,000 na ukikamilika ni 1,000.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Nzega, Adivela Bulimba, aliipongeza serikali kwa kujenga kituo cha kuweka plastiki kwenye mabomba ya kupitisha mafuta ambacho kimefungua fursa za maendeleo kwa mkoa huo.

Mratibu wa ujenzi wa mradi huo kitaifa kutoka Wizara ya Nishati, Kisamarwa Nyang'au, alisema kituo cha kuweka plastiki kwenye mabomba ya mafuta kinajengwa na kampuni za Isoaf LTD na Milembe Construction Co LTD na kitakamilika Desemba, mwaka huu.




Mkurugenzi wa M-Pesa, Epimack Mbeteni (kushoto), akipokea leseni ya kutoa huduma za bima kidijitali kwa Kamishna wa Bima wa Mamlaka ya Usimamizi wa shughuli za Bima Tanzania (TIRA), Baghayo Saqware. Vodacom inatoa huduma hizo kidijitali kupitia Voda-Bima, wateja wanaweza kupata bima za afya na vyombo vya usafiri kulipia kwa M-Pesa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jaji Kiongozi aridhishwa utendaji Mahakama Kuu Divisheni Kazi

**Na Grace Gurisha**

JAJI Kiongozi, Mustapha Siyani, amesema utendaji wa Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi umeongezeka na mrundikano wa kesi mbele ya majaji umepungua.

Jaji Siyani alisema hayo jana wakati akifungua kikao cha Utatu kwa madhumuni ya kushirikiana na Mahakama ya Kazi na kuwaleta pamoja wadau ambao ni wafanyakazi, waajiri, wanasheria na wengine wanaohusiana na migogoro ya kazi. Alisema wadau wanatakiwa kuendelea kushirikiana na mahakama kuhudhuria kesi ili kuongeza tija na namna nzuri ya upunguzaji wa mrundikano wa mashauri mahakamani na kuhakikisha haki inatendeka kwa wakati.

"Jukumu la wadau ni kuwasilisha kumbukumbu muhimu za mashauri kama vile Tume ya Usuluhisho na Uamuzi (CMA) katika Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi ili mashauri yasajiliwe na kusikilizwa kwa haraka," alisema Jaji Siyani.

Aliwataka wahakikishe waajiriwa wanapewa mikataba ya kazi na kuweka ubunifu katika utendaji ili kupunguza migogoro ya kazi na kuongeza tija za uzalishaji kwa ajili ya ukuaji wa uchumi.

"Hakikisheni kila upande unatimiza wajibu wake kwa mujibu wa matakwa ya kisheria huku mkizingatia umuhimu wa kuhakikisha kuna amani na utulivu katika maeneo yenu ya kazi," alisema Siyani.

Aliwataka wadau hao kuwa wabunifu wa kazi na madai yanayohusu fidia yashughulikiwe kwanza kwa kutoa fidia kabla ya kufika mahakamani.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Divesheni ya Kazi, Salma Magimbi, alisema mkutano huo ni utekelezaji wa nguzo ya tatu ya mpango mkakati wa mahakama ambayo inawataka kuwashirikisha wadau ili kuleta tija ya kuboresha utoaji wa haki kwa wakati.

Alisema kwa kufanya hivyo itakuwa ni msingi bora wa utekelezaji wa majukumu huku wakiongozwa na kaulimbiu ya mwaka huu. "Mapinduzi ya nne ya viwanda matumizi ya Tehama na ushirikishwaji wa wadau katika kutatua mogogoro ya kazi".

Jaji Magimbi alisema katika kikao hicho wajumbe hujadili mafanikio na changamoto na mapendekezo kwa ajili ya utatuzi wa migogoro ya kazi kwa haraka ili kupisha shughuli za kazi ziendelee.

# Barrick yatoa gawio la bil. 200/-

**Na Faustine Feliciane,** MARA

KAMPUNI ya Barrick Gold Mine, imetoa gawio la Sh. milioni 200 kwa serikali katika kipindi cha kuanzia mwaka 2020 hadi sasa.

Akizungumza kwenye mkutano na waandishi wa habari jana, Msajili wa Hazina, Mgonya Benedicto, ambao umehudhuriwa na Rais na Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo Mark Bristol, alisema mbali na gawio hilo pia serikali imepata mapato mengine ya kodi.

Alisema rekodi zote za malipo hayo zipo serikalini na kuishukuru kampuni ya Barrick kwa ushirikiano wao pamoja na kampuni ya Twiga Mineral Cooperation inayoendeshwa na Serikali ya Tanzania.

"Fedha hizo zimelipwa kwa serikali kwa kufuata makubaliano ya mkataba, zipo fedha nyingine za kodi ambazo Barrick wanazilipa kwa serikali, hii imetokana na ushirikiano mzuri kati ya serikali na kampuni hii," alisema msajili huyo.

Naye Naibu Waziri wa Madini, Casmir Kyuki, alisema serikali inafurahishwa na uendeshwaji wa kampuni hiyo, na kuahidi kuendelea kushirikiana kwa faida ya pande zote mbili.

Naibu Waziri Kyuki, aliitaka Barrick kujenga ushirikiano na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mara, mahali ulipo mgodi wa Barrick North Mara ili kutatua changamoto zilizoko.

"Kuwe na ushirikiano kuanzia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya mpaka halmashauri, hii itasaidia kuondoa migogoro inayoibuka kati ya wananchi na mgodi," alisema Kyuki.

Alishauri kesi zilizopo mahakamani ziondolewe na kuzitatua nje ya mahakama kwa kushirikiana na ofisi hizo.

"Lakini kwa ile migogoro ya fidia, niombe Barrick iwalipe wote ambao wanastahili, pia kwa wananchi waache kudanganya kupata malipo wasiyostahili," alionya.

Akifungua mkutano huo, Rais na Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo, Mark Bristow, alisema tangu kampuni hiyo ianze kuendesha migodi ya North Mara na Bulyanhulu mwaka 2019, uwekezaji umefika thamani ya Dola za Marekani bilioni 1.995.

Pia imelipa Dola milioni 158 za Kimarekani kama kodi, mirabaha na ushuru, gawio la serikali pamoja na mikopo ya uwekezaji yenye thamani ya Dola milioni 42.

"Tulipoingia ubia na serikali na kuanza kuendesha migodi hii, ilikuwa mzigo kwa serikali na wawekezaji wao, katika kipindi cha muda mfupi tulifanikiwa kuisuka upya na kuweka ushirikiano mzuri na serikali na faida yake inaonekana," alisema Bristow.

Alisema Barrick inaendelea kuchukua hatua endelevu kwenye maeneo wanayochimba madini na kuhifadhi mazingira katika migodi yote miwili na North Mara na Bulyanhulu na wanalenga kutoa fursa mpya.

"Katika hili tumeendelea kujiimarisha katika maeneo ya Bulyanhulu kutokana na kupata leseni sita za kutafiti madini katika maeneo yanayopakana jirani na mgodi huo," alisema Bristow.

Kwa upande wake, Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara, alisema mgodi wa North Mara unazungukwa na vijiji 11 na wanaishukuru Barrick kwa ushirikiano.



Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, akizungumza katika mkutano wa waandishi wa habari na Rais na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Barrick, Mark Bristow (kulia), kuhusu uwekezaji wa kampuni hiyo kwa migodi ya Bulyanhulu na North Mara kuwa umefikia thamani ya dola za kimarekani bilioni 1.995, mkoani Mara jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Anayedaiwa jambazi sugu wa mauaji auawa

**Na Neema Hussein,** KATAVI

JESHI la Polisi Mkoa wa Katavi, limemuua kwa risasi Heleni Nyankole (36), maarufu Beberu, mkazi wa Kijiji cha Kapanga wilayani Tanganyika, anayedaiwa kuwa kinara wa mauaji ya kukodiwa ndani na nje ya mkoa huo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Ali Makame, alisema mtuhumiwa huyo aliuawa wakati alipojaribu kuwakimbia askari.

Alisema Juni 28, mwaka huu, majira ya saa 5:30 usiku, Nyankole anadaiwa kumshambulia Mandalu Ndulu (36), mkazi wa Kijiji cha Bukombe, wilayani Tanganyika kwa kumkata na kitu chenye ncha kali shingoni na kumsababishia kifo.

Kamanda alisema wakati wa uhai wake, Nyankole anadaiwa kukodiwa na Emmanuel Dila na Jitale Mwigulu, wakazi wa kijiji cha Luhita-Bujombe kwa makubaliano ya kumlipa Sh. 800,000, ili amuue Mandalu kwa kinachodaiwa tukio linalohusishwa na wivu wa kimapenzi.

Akifafanua kuhusu tukio hilo, Kamanda Makame alisema polisi baada ya kupata taarifa waliwakamata watuhumiwa hao wawili na baada ya kuwahoji walikiri kumkodi muuaji huyo, ambaye walimpa malipo ya awali ya Sh. 300,000 na kutekeleza tukio hilo.

"Tulianza msako mkali Julai 7, mwaka huu, majira ya saa 9:00 usiku, tulimkamata muuaji Kijiji cha Lwega, wilayani Tanganyika akiwa amelala nyumbani kwake, polisi walipomuamuru kujisalimisha alikaidi," alisema.

"Alipanda juu ya dari kisha kutoboa paa la nyumba iliyoezekwa kwa nyasi kwa kutumia panga, akiwa juu ghafla alishuka akiwa na kipande cha nondo kwa lengo la kumjeruhi askari," alisema.

Kamanda alisema askari walifyatua risasi hewani ili kumuonya, lakini alikaidi na kuendelea kuwafuata, walifyatua nyingine ikamjeruhi tumboni na kupoteza maisha wakati anakimbizwa kituo cha afya.

Alisema jeshi hilo lilikuwa likimtafuta mtuhumiwa huyo kwa muda mrefu akihusishwa na tuhuma za kujeruhi watu kwa mapanga.

## 23 wachukua fomu kuwania uongozi CCM mkoani Mara

**Na Samson Chacha,** MARA

WANACHAMA 23 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), mkoani Mara wamechukua fomu za kuwania nafasi mbalimbali, ikiwamo 10 wanaotaka uenyekiti wa mkoa.

Katibu huyo wa CCM Mkoa wa Mara, Langael Akyoo, aliwataja wagombea hao kuwa ni mwenyekiti wa sasa

Samwel Kiboye na Patrick Chandi, Daud Ngicho, Mirumbe Joshua, Nyerere Jackson na Paschal Regu.

Wengine ni Magori Mgalani, Juma Khamis, Ziara Munasa Sabi, Christopher Sanya, Charles Masatu, Flora Mundeba, Kagion Zongori, Maulid Shaban, Icone Mjarufu, Leonard Kitwara, John Marande, Kyabwene Misana, Silvanus Msore, Emmanuel Mngarwe, Abednego Range na Samwel Alfred.

Wanachama 14 waliochukua fomu za kuwania Ujumbe wa Halmashauri Kuu CCM Taifa ni Christopher Mwita Gachuma kutoka Tarime anayetetea nafasi hiyo.

Wengine ni Juma Khamis, Ismail Masuruli, Franko Buberwa, John Oboto, Abdalh Mlaima, Jumma Mokili, Daniel Mbuba, Adam Misango, Ramadhan Chacha, Erenest Makanya na Haji Mgeta.

**Wanachama 14 waliochukua fomu za kuwania Ujumbe wa Halmashauri Kuu CCM Taifa ni Christopher Mwita Gachuma kutoka Tarime anayetetea nafasi hiyo.**

# Simba Gas kuchimba hewa ukaa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Kitanzania ya Simba Gas, inajiandaa kuanza kuchimba gesi ya ukaa (Carbon dioxide), huku ikilenga kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya bidhaa hiyo katika soko la ndani na nje.

Uchimbaji utaanza baada ya kupata vibali vyote vya udhibiti kutoka katika taasisi zote zinazohusika, baada ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), kukamilisha utafiti wa miezi miwili uliofanywa na wataalamu katika kata ya Suma, wilayani Rungwe, mkoani Mbeya.

Simba Gas ilisajiliwa mwaka 2021 kama sehemu ya kundi la kampuni ya Simba ikijikita katika kuchimba na kuuza gesi ya ukaa mwishoni mwa wiki imepokea matokeo ya utafiti kutoka Kitivo cha Jiologia na Madini cha UDSM.

Gesi ya ukaa hutumika kutengeneza vinywaji vyenye gesi, kipoozo katika vizima moto kwa kuingizwa katika vifaa vya uokoaji na uchomeleaji vyuma katika miradi mikubwa.

Pia kutengenezea barafu kavu zinazotumika kupozea vinywaji, ulipuaji wa makaa ya mawe, utengenezaji wa vifaa vya mpira na plastiki, ukuzaji wa mimea katika vitalu nyumba na pia kupunguza nguvu za wanyama kabla ya kuchinjwa.

Akiongea wakati wa hafla ya kupokea ripoti ya utafiti, Mkurugenzi wa Kampuni Simba Gas, David Ndelwa, alisema soko la gesi ya ukaa linakua kwa kasi kubwa ndani na nje ya nchi.

"Kwa sasa mahitaji ya gesi ukaa katika soko la ndani yanafikia tani 1,060 kwa wiki na tunao upungufu wa tani 360 kwa wiki," alifafanua.

Vile vile, mahitaji ya soko la mauzo ya nje la gesi ya ukaa kwa sasa ni takribani tani 2,000 upungufu ni tani 1,460.

"Inakadiriwa kuwa hadi sasa, soko la kimataifa la gesi ukaa linafikia thamani ya Dola bilioni 10.36. Kampuni yetu imejiandaa vya kutosha na itawekeza kwa kiasi kikubwa ili kuhakikisha kuwa tunatumia rasilimali tulizo nazo kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi," alisema Ndelwa.

Alisema kampuni hiyo imefanya utafiti na kuona soko kubwa la gesi ukaa lipo nchi za Zambia, Zimbabwe, Congo, Malawi, Msumbiji, Afrika Kusini, Botswana, Angola, Sudan Kusini, Rwanda na Namibia.

"Tunatambua kwa kusafirisha gesi yetu nje ya nchi, tutaleta fedha za kigeni nchini. Pia tutazalisha nafasi za ajira za moja kwa moja 150 na zingine 300 za muda maalum," alisema.

Alibainisha kuwa utafiti zaidi utalazimika kufanyika ili kukidhi matakwa ya kimataifa ya uvunaji wa bidhaa hiyo na ameiomba serikali kuendelea kuweka mazingira mazuri yatakayovutia ufadhili zaidi wa shughuli hizo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Zuberi Homera, alisema serikali inajitahidi kuboresha mazingira ya biashara na kuvutia uwekezaji katika sekta ya nishati na viwanda miongoni mwa mambo mengine.

"Mradi huu utakapoanza rasmi, utazalisha ajira, kuongeza mapato ya serikali za mitaa na kusaidia jamii kupitia mipango ya uwajibikaji kwa jamii. Serikali itaendelea kuunga mkono uwekezaji huo," alisema.

Naye Mkuu wa Kitivo cha Jiolojia na Madini wa UDSM, Dk. Elisante Mshiu, aliwashukuru kampuni ya Simba Gas kwa kuwaamini wataalamu wa ndani ambao wamejikita kuleta ukombozi na mageuzi makubwa ya kufanya tafiti za kimkakati na kuhakikisha taifa linanufaika na rasilimali zake.

# Kairuki yaweka kambi kutoa elimu ya afya ya akili

**Na Joseph Mwendapole**

IDARA ya Ustawi wa Jamii ya Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU) kwa kushirikiana na Hospitali ya Kairuki, wameandaa kambi ya mwezi mmoja kwa ajili ya kutoa ushauri na elimu ya afya ya akili.

Huduma hiyo inatolewa bure katika viwanja vya maegesho Mlimani City jijini Dar es Salaam na itaendeshwa kwa mwezi huu wote kwa siku za Alhamisi, Ijumaa na Jumamosi.

Mkufunzi wa Idara ya Ustawi wa Jamii wa (HKMU), Esther Katende, aliliambia gazeti hili jana kuwa wameona watoe huduma hiyo baada ya kubaini kuwa tatizo hilo linazidi kuongezeka.

"Tumeona ni vyema kuandaa mwezi wa afya ya akili baada ya kuona tatizo linaongezeka na matukio mengi ya mauaji yanazidi kushamiri sehemu mbalimbali nchini hivyo tumeona jamii inahitaji huduma muhimu ya ushauri," alisema.

Alisema, pia wanapima afya kwa ujumla kwa watu wote watakaojitokeza kwenye kambi hiyo na kuwapa ushauri wa kitaalamu watakaokutwa na shida mbalimbali.

"Viashiria vya tatizo la afya ya akili viko vingi, mojawapo ni kujitenga au kutengwa, ukimya usio wa kawaida, mabadiliko katika mtiririko wa mawazo, maongezi na matendo hivyo basi viashiria hivi vikionekana kwa mtu awahishwe kwa wataalamu ili kupata msaada mapema," alisema.

"Idara ya Ustawi wa Jamii ya Hubert Kairuki Memorial University, pamoja na vyuo vingine vinavyotoa elimu ya Ustawi wa Jamii ni chimbuko mojawapo la wataalamu wanaotoa huduma kwa wagonjwa wa aina hiyo," alisema Esther. Aidha, aliwakaribisha watu wote kupata ushauri na elimu kuhusu afya ya akili pamoja na upimaji afya katika viwanja hivyo, ili waweze kufahamu vyema kuhusu afya zao na kama watabainika kuwa na tatizo wawahi mapema kulitatua.

Taarifa ya mwaka jana ya Shirika la Afya Duniani (WHO), katika siku ya afya ya akili duniani ambayo kila mwaka huadhimishwa Oktoba 10, ilisema mzigo wa matatizo ya afya ya akili miongoni mwa vijana unasababisha msongo wa mawazo na hatimaye kujiua.

Ilisema vitendo vya kujiua ni sababu inayoshika nafasi ya pili kwa vifo vya vijana kati ya umri wa mika 15-19 na tatizo linaloongoza ni matumizi mabaya ya pombe na mihadarati hali inayosababisha matatizo ya akili kuwa moja ya changamoto kubwa kwa nchi nyingi duniani.

Kwa mujibu wa WHO athari za kutoshughulikia matatizo ya afya ya akili kwa vijana ni kubwa na mara nyingi zinaendelea hadi ukubwani na kuwakosesha fursa ya kufanikiwa katika maisha yao kutokana na msongo.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, kwenye ujumbe wake wa Siku ya Afya ya Akili Duniani mwaka jana, alisema ni muhimu serikali zikawekeza zaidi kwenye sekta za afya, elimu na jamii.

Alisema hiyo itasaidia kudhibiti janga hilo kuhakikisha ajenda ya 2030 ya maendeleo haimuachi yeyote nyuma, ikiwamo vijana wenye matatizo ya akili ambao hunyanyapaliwa na kukosa msaada wakati mwingine.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya DCB, Godfrey Ndalahwa, akizungumza na wajumbe katika mkutano ulioandaliwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Saada Mkuya (hayupo pichani), ukiwashirikisha wakuu wa taasisi mbalimbali za fedha za Tanzania Bara na Visiwani kujadili fursa za kifedha zipatikanazo katika kampeni ya uchumi wa buluu iliyoasisiwa na Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, mjini Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Machinjio ya kisasa Nyakato yakosa maji

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAFANYABIASHARA katika machinjio ya kisasa ya ng'ombe ya Nyakato, wilayani Nyamagana, wanalazimika kwenda na ndoo za maji kwa ajili ya kuoshea nyama kutokana na huduma hiyo kukosekana kwa wiki tatu.

Machinjio hayo yaliyogharimu zaidi ya Sh. milioni 900, hayana huduma ya maji, mashine ya kuchinjia mifugo, eneo la kushushia ng'ombe na uzio.

Akizungumza na wafanyabiashara hao katika machinjio hayo, Meya wa Jiji la Mwanza, Sima Constantine, alikiri kuwapo tatizo hilo na kuahidi kutatua.

Alisema atazungumza na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mkoani Mwanza (MWAUWASA), ili kuhakikisha maji yanapatikana muda wote katika machinjio hayo.

Aidha, aliahidi kuzungumza na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), ili kuboresha miundombinu ya eneo hilo na upande wa uzio atazungumza na Mkurugenzi wa Jiji atenge bajeti pamoja na kuweka mashine za kuchinjia.

Meya huyo aliyetembelea machinjio hayo saa 10 usiku, alishuhudia wachinjaji wakifanya kazi katika mazingira magumu kutokana na kukosa huduma muhimu ikiwamo maji.

Alisema huduma ya maji ilikuwapo, lakini imekosekana kutokana na bomba kubwa linalopeleka eneo hilo kukatika kwa zaidi ya wiki tatu.

"Leo mapema (jana) nitaongea na viongozi wa MWAUWASA juu ya namna ya kutatua tatizo hili kwa haraka kwa kuwa limesababishwa na kupasuka kwa bomba kubwa linaloleta maji katika machinjio hii ili kuponyesha afya za watu," alisema Sima.

"Kwa upande wa miundombinu mwenyewe nimeliona nitaongea na watu wa TARURA ili kuweza kurekebisha miundombinu hiyo ili iwe rafiki katika utendaji kazi katika machinjio hii," alisema.

Wakitoa kilio chao mbele ya Meya, baadhi ya wafanyakazi na viongozi wa machinjio hayo, waliiomba serikali kutatua tatizo hilo kuepusha madhara ya kiafya katika jamii.

"Tumekuwa tukitaabika sana kutokana na ukosefu wa maji kwa zaidi ya wiki tatu sasa hatua inayotupa wakati mgumu sana na kulazimika kutoka nyumbani na ndoo za maji ili kusafishia nyama na sehemu tunazofanyia kazi hali ambayo siyo salama kwa afya zetu na watumiaji pia," alisema Francis Kinyundo Kwa upande wake, mfanyakazi James John, alisema licha ya machinjio hayo kuwa ya kisasa, hakuna mashine za kuchinjia ng'ombe.

"Tunapata wakati mgumu kuhakikisha eneo hili la machinjio linakuwa salama kwa kuwazuia watu wasiingie ndani, lakini changamoto inabaki kuwa hakuna uzio hivyo watu hupita sehemu tofauti, vilevile licha ya machinjio hii kuwa kubwa bado hatujawekewa mashine za kisasa kwa ajili ya kuchinjia," alisema.

Akizungumza na waandishi wa habari waliofika eneo hilo, Meneja wa machinjio hayo, Kamilius Bajuga, alikiri kuwapo tatizo hilo kwa muda mrefu.

Ujenzi wa machinjio hiyo ulikamilika Agosti 15, mwaka 2018.

Rais Samia Suluhu Hassan wakati huo akiwa Makamu wa Rais, aliwahi kuagiza Halmashauri ya Jiji la Mwanza kufunga mashine za kisasa, lakini mpaka sasa hazijafungwa.

HABARI ZA MAONYESHO DITF

# Wajasiriamali bidhaa za uokaji wapewa njia kujitangaza

Na Elizabeth Zaya

MKE wa Waziri Mkuu mstaafu, Tunu Pinda, amewashauri wajasiriamali wa bidhaa za kuokwa, kutumia majukwaa makubwa ya kibiashara kutangaza bidhaa zao.

Aliwashauri pia kutumia teknolojia ya kidijitali kutangaza bidhaa hizo huku akiwataka kuziboresha zaidi kupambana na ushindani katika soko.

Alikuwa akizungumza na wanachama wa Chama cha Waokaji (TBA), kwenye Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF) yanayoendelea kwenye viwanja vya Sabasaba.

Aliwashauri wanachama hao kuandaa siku maalum ya mafunzo ya uokaji ili kutoa fursa ya kubadilishana uzoefu na namna ya kukuza soko la bidhaa zao.

Mwenyekiti wa chama hicho, Francisca Lyimo, aliiomba serikali kupunguza gharama za bidhaa wanazotumia katika bidhaa za kuoka.

Alisema kupanda kwa kodi, unga na mafuta ni changamoto kubwa kwa wafanyabiashara hao.

"Chama chetu kinakabiliwa na changamoto kubwa ya kupanda kwa gharama za vifaa kama unga na mafuta na kuchangia kupungua kwa soko la uzalishaji," alisema Francisca.

Alisema chama hicho kiko tayari kuungana na SIDO kutoa mafunzo ya uandaaji wa kuoka mikate hiyo kwenye kiwango kinachotakiwa.



Ofisa Uwekezaji wa Shirika la Umeme TANESCO, Patrick Mwakyoma (wa pili kushoto), akiwaelekeza wananchi waliotembelea banda lao kujionea hatua ya mradi wa bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere katika Maonyesho ya 46 ya Kimataifa Sabasaba barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ufugaji ng'ombe kisasa wapigiwa chapuo

MENEJA Masoko wa Kampuni za Ranchi za Taifa, Mnzava Emmanuel, ametoa ushauri kwa Watanzania wanaopenda kuwekeza kwenye ufugaji wa kisasa wa ng'ombe wanaokuwa kwa muda mfupi na kibiashara ili kuviwezesha viwanda vinavyofanyakazi kwa kutegemea bidhaa hiyo kutokosa malighafi.

Alisema Tanzania imejenga machinjio mengi, lakini baadhi yake yanajiendesha chini ya uwezo kutokana na kutokuwa na malighafi nyingi mengi.

"Tunasisitiza ufugaji wa kisasa na wa kibiashara ambao miaka miwili tayari ng`ombe anakuwa ameshafika kilo 400 kwa ajili ya kupelekwa sokoni, na hicho ndicho tumekuja nacho Sabasaba kuwaambia Watanzania," alisema Emmanuel.

Alisema katika maonyesho hayo, wana mbegu ya ng'ombe aina ya Borani ambaye ukuaji wake ni wa muda mfupi ambayo wanasisitiza itumiwe na wafugaji na tayari wametoa ofa ya punguzo la bei kwa kipindi chote cha maonyesho hadi Julai 20, mwaka huu ili kusaidia Watanzania wengi kupata.

"Tuna machinjio ambayo yamejengwa nchini na yanaendelea kujengwa, yanaendeshwa chini ya uwezo wake wa kuchakata kwa sababu pamoja na kwamba mifugo iko mingi, lakini viwanda bado vinakosa mifugo. Kwa hiyo tunataka wachukue mbegu hizi ili mifugo ikue ndani ya muda mfupi na waipeleke viwandani ili viweze kufanya kazi ya kuzalisha bila kukosa malighafi," alisema Emmanuel.

"Katika Sabasaba hii tumekuja na ofa kubwa ya ng'ombe dume aina ya Borani kwa ajili ya Watanzania ambayo ni punguzo la asilimia 14 kutoka kwenye bei ya awali na imeanza tangu kipindi cha maonyesho haya na itadumu mpaka Julai 20, mwezi huu."

Tangu wametoa ofa hiyo, mwitikio wa wafugaji umekuwa mkubwa na wanaangalia namna ya kupeleka tena ofa hiyo katika maonyesho ya Nanenane ili kuwezesha wananchi wengi kupata mbegu ya ng'ombe hao.

"Wananchi wengi wenye makundi ya mifugo, wamekuwa wakipiga simu na tunawapa control namba wanaenda kwenye ranchi, wanalipa fedha na wanachukua madume yao kwenda kwenye mikoa mbalimbali nchini kwa ajili ya kwenda ku upgrade kwenye majike yao,"

"Na uki upgrade kwenye majike ya asili, matokeo yake ni kwamba utapata machotara wa ng'ombe wanaokua kwa haraka na kwa muda mfupi, tayari kwa kupelekwa sokoni."

Vilevile, wana fursa za uwekezaji wa kimkakati wa viwanda vya kuchinja ng'ombe, kuchakata nyama, maziwa, malisho, ngozi, mazao ya ngozi ikiwamo mikanda, makoti na mabegi.

"Kama yupo Mtanzania ambaye anafikiri anaweza kuwekeza kimkakati na uwekezaji wake ukaleta matokeo na faida kwa wananchi wengi, maeneo ya kuwekeza kwenye viwanda hivyo kwenye mnyororo mzima wa thamani yanapatikana kwenye ranchi zetu za taifa ambazo kwa ujumla ziko 14 na karibu katika kila kanda kuna ranchi moja au mbili," alisema Emmanuel.

# Wanafunzi wagundua mfumo utoaji taarifa tatizo la umeme

WANAFUNZI wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), katika kitivo cha Information and Communication Technology Co ICT, wamegundua mfumo maalum ambao utasaidia kurahisisha utoaji wa taarifa kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kuhusua tatizo la umeme kwenye transfoma na laini za umeme.

Akizungumza na Nipashe, Mtafiti Msaidizi wa mradi wa mfumo huo, Nelson Kimaro, alisema ugunduzi huo utakuwa na mfumo maalum katika kompyuta ambao utawekwa katika ofisi za TANESCO na pia kutawekwa kifaa maalum kwenye transfoma ambacho kitakuwa kinakusanya taarifa inapotokea shida kitazituma kwenye mfumo huo wa shirika.

"Huu mfumo utakuwa na ramani ambayo inaonyesha sehemu zote ambazo zina transfoma na kwenye hiyo ramani inapotokea kuna ambayo imepata shida itatoa taarifa kwa kuonyesha rangi nyekundu na meneja anapopata taarifa hiyo atakwenda kwenye mfumo na kumpeleka fundi kwenda kufanyia kazi. Mfano taarifa anayopata ni kwamba transfoma fulani ya Mwenge ina shida katika line ya tatu na ni shida ya namna gani, labda umeme umezidi sana au upo chini, umekatika katika laini hiyo au kiwango cha mafuta kimepungua," alisema Kimaro.

Mradi huo unalenga kuboresha zaidi mifumo ya usimamizi wa transfoma za TANESCO hususani inapotokea shida katika transfoma za mitaani.

"Mradi huu unalenga tutatua tatizo pale linapotokea tatizo linalohusiana na transfoma kule mitaani muda huo huo unatoa taarifa kwa TANESCO kwamba ni tatizo gani limetokea na ni katika transfoma gani, eneo ambalo transfoma ipo," alisema Kimaro.

"Hii inasaidia kurahisisha mawasiliano kati ya transfoma zenye shida na uongozi wa TANESCO. Ukiangalia kwa sasa ikitokea tatizo lolote kwenye mfumo wa usambazaji umeme wa shirika hilo hususani kwenye transafoma huwa wanapata taarifa mpaka pale mteja au mwathirika apige simu au awafuate ofisini kwao ili wakarekebishe."

"Na muda mwingine ni process (mchakato) ambayo inachukua muda mrefu mpaka tatizo kutatuliwa na hata kuchangia kupunguza uzalishaji kwa mtumiaji wa huduma. Kwa hiyo kupitia mfumo huu taarifa itakuwa inatolewa muda huo huo baada ya tatizo kutokea, kwamba kuna shida katika transfoma fulani na ni ya namna gani."

# Watanzania wapata hamasa kutoa elimu sekta mafuta, gesi

WATANZANIA wanaotoa huduma za kitaalamu katika sekta ya mafuta na gesi wamesema ushiriki wao katika maonyesho ya 46 ya biashara ya kimataifa, umewapa hamasa ya kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na umuhimu wa wazawa kuingia katika sekta hiyo.

Akizungumza na Nipashe kwenye banda la Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), kama miongoni mwa wazawa wanaotoa huduma ambayo mamlaka hiyo imewapa nafasi ya kuonyesha mfano kuhusu fursa zinazopatikana katika sekta hiyo akitokea kampuni ya Solution tag Consulting Co. Ltd, Peter Chuwa, aliwashauri Watanzania wasiogope kuingia kwenye sekta hiyo.

Alisema Watanzania wengi wanaogopa kuingia katika sekta hiyo wakiamini kwamba ni ngumu na kuwaachia wageni.

"Tunashiriki katika maonyesho haya kama kampuni ya wazawa ambao tumepewa nafasi na PURA kuonyesha mfano juu ya fursa zilizopo katika sekta ya mafuta na gesi, tunachoona ni kwamba bado Watanzania wenzetu hawana udhubutu wa kuingia katika sekta hii, wengi wanaona ni ngumu, wanaamini kwamba wageni ndio wana uwezo wa kuifanya kuliko wao, hii siyo sahihi na ndiyo maana tuko hapa kuwaelimisha," alisema Chuwa.

"Ninachotaka kuwaambia ni kwamba sekta hii haina ugumu wowote ni kujiamini. Na ushiriki wetu kwenye maonyesho haya mwaka huu umeendelea kutupatia fursa ya kutambulika, lakini ninaamini kwamba wengi waliokuja kututembelea wamejifunza na kubadili mtizamo wao kuhusu kushiriki katika sekta hii ya mafuta na gesi."

Alisema miongoni mwa maswali wanayoulizwa kutoka kwa wengi wanaowatembelea katika banda lao ni endapo kuna faida yoyote wanayoipata kufanya shughuli za mafuta na gesi.

"Wananchi wengi wanaotutembelea wanataka kujua ushiriki wetu katika sekta ya mafuta na gesi, wanataka kujua huwa tunafanya nini, na tunafaidikaje na sera ya ushirikishwaji wa kampuni za wazawa kwenye sekta hiyo," alisema Chuwa.

"Tunashukuru pia viongozi wa serikali waliotutembelea walitutia moyo na kutushauri kuongeza juhudi ili tufikie viwango vya kimataifa katika kutoa huduma za kitaalam sekta hii ya mafuta na gesi.

Alisema ni vyema Watanzania wenye uwezo wa kifedha na taaluma inayohusiana na sekta hiyo, kuwa na uthubutu wa kushiriki kuanzisha kampuni ili wachangie maendeleo ya nchi.





Ukurasa 12

## Tiba migogoro ya ndoa, unyanyasaji imepatikana


Nipashe

# TESA

Jumanne Julai 12, 2022

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI




Ukurasa 13

## Uganda yafurahia, yaizawadia Siku ya Kiswahili Duniani waraka maalum

ELIMU
NA MWANDISHI
WETU

# Majeruhi kuuawa, kuporwa, maiti kupekuliwa

• CHAKUA yaelekeza CCTV, sheria, kushtaki

AJALI za barabarani zimeua na kujeruhi wengi, lakini kwa wanaopata ajali ni kama kufikwa na janga mara 10. Inamaanisha kuwa katika mkasa huo, kuna kunusurika lakini ukanyongwa na kuibiwa mali au shehena na hao 'Wasamaria wema' wanaolenga kutajirika kupitia ajali.

Pamoja na kuibia majeruhi, wafu nao hawajaachwa wanakapekuliwa na kuporwa mali na mwishowe licha ya kuwa watu waliojulikana, wanaweza kuzikwa na serikali kwa sababu miili haikutambuliwa, kwa sababu hawakuwa na vitambulisho.

Juhudi za kupunguza ajali hizo, zinafanywa na Kikosi cha Usalama Barabarani, askari wakiwatoza faini na kuwafungia leseni madereva wanaohusika na hivi karibuni, Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Wilbroad Mutafungwa, anazindua mafunzo ya elimu kwa madereva na abiria kwenye vituo vya mabasi.

Elimu hiyo inalenga kuuelimisha umma kuhusu kupunguza ajali hizo.

Wakati wa uzinduzi wa elimu hiyo unaofanyika jijini Dar es Salaam kwenye stendi kuu ya Magufuli Mbezi, anawataka madereva kuwa makini barabarani ili hata ajali inapotokea isisababishe madhara makubwa.

Wakati mafunzo hayo yanaendelea, suala la ajali hizo kuwa 'janga mara 10' kwa wafu na wanaonusurika linahitaji pia kutazamwa. Abiria hao wanakutana na wezi wanaojifanya 'Wasamaria wema' wanaowahudumia lakini kinachoendelea ni kuiba na si kuokoa maisha wala kulinda mali za waliopata ajali.

Kuna visa vingi ikiwamo ajali iliyotokea eneo la External Dar es Salaam, mwanafunzi wa chuo kikuu jina tunalo, alikuwa na Shilingi 4,000,000 kulipa ada ya chuo, kodi ya nyumba na fedha za matumizi ambazo ziliporwa bila huruma.

Anasema aliamua kupanda bodaboda hadi kuelekea chuoni eneo la Mikocheni lakini pikipiki hiyo iligongwa na gari la mizigo lililokuwa likiendeshwa kwa kasi likasababisha ajali iliyomvunja mguu wa kulia na dereva kuumizwa pia.

"Mmoja wa watu wa kwanza waliofika eneo la tukio hakuniambia hata pole, aliondoka na begi langu na kila kitu kilichokuwamo. Nikamwambia usichukue begi langu, akaniambia umeumia utakufa huwazi ya Mbingu siyo mali..." anasema majeruhi huyo.

Matukio ya kuwanyonga na kuwaibia majeruhi na kuwapekua maiti, lakini baya zaidi kuwamalizia au kuwaua watu ambao wamenusurika ili kuchukua mali zao ni jambo linalosikika sana.

Lakini, si hivyo tu hata wenyeji hukimbilia kupora kutoka kwenye malori yanayosafirisha vyakula, pombe na mafuta pale ajali inapotokea.

Mkoani Morogoro Agosti 2019, wakati Wilbroad Mutafungwa, akiwa Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, alishuhudia watu zaidi ya 60 wakifariki na wengine kadhaa takribani 70 wakijeruhiwa baada ya lori la mafuta kugonga bodaboda eneo la Mzambarauni karibu na stendi ya Msamvu na kuanguka.

Hata hivyo, kilichowaua si gari kuanguka bali watu walifariki kwa kuungua na moto uliotokana na kuchangamka kutafuta petroli baada ya lori lililokuwa likisafirisha mafuta hayo kupinduka karibu na stendi.

Watu walitapakaa katika eneo la tukio wakiwa na madumu, chupa na mifuko ya nailoni, wakichota petroli kutoka kwenye lori bila kujali hatari. Yote hayo ni kwa sababu ya desturi za wizi na kupenda kuiba kwenye ajali, kupora majeruhi na kupekua maiti.

Barabara ya Morogoro inayoanzia Dar es Salaam hadi Tunduma ni sehemu maarufu kwa usafirishaji wa abiria, shehena kuanzia vyakula, mbao hadi mafuta na pia ni eneo linalotikisa kwa ajali za barabarani.

Licha ya kwamba hakuna takwimu zinazozungumzia ukweli wa mambo, lakini Hospitali ya Tumbi iliyoko Kibaha inapokea majeruhi na miili ya ajali za barabarani mara kwa mara.

Kuna madai kutoka kwa wakazi wa maeneo ya Chalinze hadi Kibaha kuwa kuna vijana ambao wako macho kila mara na wameunganishwa na mitandao kiasi kwamba inapotokea ajali wanakuwa wa kwanza kufika eneo la tukio na kufanya uhalifu.

Vijana hao wanajifanya wasamaria wema kusaidia, badala yake huwapora majeruhi, huwamalizia wanaoleta ubishi, hupekua miili na kuiba, wanaligeukia gari na kuiba vifaa kama taa, matairi, vioo, betri na hali inakuwa mbaya kama ni usiku hata viti huibwa, yote hayo hufanyika kabla ya polisi kufika.



Ajali zinapotokea wahalifu wanaojifanya wasamaria wema huwaadhibu zaidi waathirika badala ya kuwasaidia. **PICHA: MTANDAO**

**VINAVYOLENGWA**

Kwa mujibu wa taarifa za uporaji abiria wa ajali, wezi wanalenga zaidi simu za mkononi, pesa, vitu vya thamani kama saa hereni na pete zikiwamo za ndoa, mizigo hasa mabegi ya abiria.

Wanaiba pia vyakula kama soda, pombe, mchele, mafuta, magunia ya viazi mahindi. Lakini lipoanguka gari la mafuta nayo pia huibiwa. Tabia hiyo 'hatari' si kwamba imeanza leo imekuwapo na inaendelea kukua.

Kikosi cha Usalama Barabarani kinapopambana na ajali za barabarani ni wakati pia wa kubuni mbinu za kudhibiti wizi wa kuwaibia na hata kuwaua majeruhi, kuibia wafu na kupora vifaa vya

INAENDELEA UK.14

ELIMU
NA SABATO
KASIKA

# Tiba migogoro ya ndoa, unyanyasaji kijinsia wanawake, watoto imepatikana

• Taasisi kufikia kila mhitaji shuleni hadi mitaani

TAASISI ya Ustawi wa Jamii, imeelekeza nguvu zake katika utoaji wa elimu ya makuzi na malezi, ushauri na msaada wa kisaikolojia kwa wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na watu wengine ndani ya jamii.

Hatua hiyo inaelezwa na Mkuu wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Dk. Joyce Nyoni, kuwa inatokana na changamoto mbalimbali katika jamii na matukio mengi ya ukatili wa kijinsia na migogoro ya kifamilia

Anataja changamoto nyingine kuwa ni migororo katika familia na hata sehemu za kazi, na kwamba kituo hicho kina wajibu wa kutoa elimu, kushauri na kusaidia kisaikolojia kama njia mojawapo ya kuondoa changamoto hizo.

Dk. Nyoni anasema hayo kwenye banda la taasisi hiyo, kwenye viwanja vya Sabasaba, jijini Dar es Salaam ambako kituo hicho kinaendelea kutoa huduma mbalimbali zikiwamo za elimu kwa wanaowatembelea kwenye maonyesho.

"Ni kituo kinachotoa ushauri kama lilivyo jina lake, kinatoa elimu, ushauri na msaada wa kisaikolojia, tunaposema elimu maana yake tunatoa elimu ya makuzi na malezi ya watoto, elimu ya mahusiano," anasema Dk. Nyoni.

Anafafanua kuwa, kupitia Kituo cha Elimu, Ushauri na Msaada wa Kisaikolojia cha taasisi hiyo, wanazungumza na wanafunzi katika shule za msingi, sekondari na kuwapa ujuzi ambao utawasaidia katika kukua kwao.

"Hatuishii hapo tu bali pia kwa wanafanyakazi na jamii, kwa upande wa msaada wa kisaikolojia tunamrudisha mtu katika hali ambayo anaweza kuwa na manufaa katika jamii," anasema.

Dk. Nyoni anawataka watu walio na changamoto ya msongo wa mawazo wanaweza kukimbilia katika kituo hicho, Kijitonyama katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii au maofisa ustawi wa jamii.

**WITO KWA WAZAZI**

Anawataka wazazi na walezi kuhakikisha wanatenga muda wa kutosha kuzungumza na watoto wao, ili kujadili masuala mbalimbali kwa lengo la kuwaepusha wasiingie katika changamoto zikiwamo za ukatili wa kijinsia.

"Pamoja na hayo wazazi wanapaswa kuwafanya watoto kuwa marafiki wao na kutumia muda mwingi kuzungumza nao, kwa kufanya hivyo watoto wanaweza kujenga mahusiano ya karibu na wazazi wao," anasema.

Dk. Nyoni pia anawataka wazazi kufikisha taarifa sahihi kwa watoto wao, vinginevyo watoto wanaweza kuzitafuta kwingine hali ambayo inaweza kusababisha wakapotoka kimaadili na kujiingiza katika vitendo visivyofaa.

"Kama mzazi atakuwa na mahusiano ya karibu na mtoto, hata akikutana na mtu ambaye si mwema, atarudi kwa mzazi na kumweleza mazingira aliyokutana nayo bila kificho," anasema.

Anaongeza kuwa ni muhimu kutafuta fedha, lakini fedha isiwe zaidi ya malezi, bali watoto wawe wa kwanza, ili wanapokutana na changamoto warudi kwa wazazi na kuwaeleza, ili wasaidiwe.

"Katika eneo la ukatili wa kijinsia, hakuna takwimu za kisayansi, bado hatujafanya utafiti, lakini kwa kuangalia kwa haraka haraka tatizo ni kubwa kwani hata ukiangalia katika familia nyingi utabaini hali ilivyo," anasema.

Aidha, anataja changamoto anayoiona katika jamii kuwa ni watu kutotambua kuwa kuna msaada kuhusu yale ambayo yanawakabili, na kwamba kijana anaweza kupata tatizo katika mahusiano akakata tamaa ya maisha, kumbe kuna mahali anaweza kwenda akatatuliwa kile kinachomsumbua.

**KUANZA KWA KITUO**

Kwa mujibu wa Mkuu wa Taasisi, huduma za ushauri zilianza mwaka 2007 kupitia kituo wakati huo kikiitwa Counseling and Information Center, ambapo kilitoa huduma kwa jamii iliyokuwa inawazunguka.

Huduma hiyo ilitolewa pia kwa wafanyakazi na wanafunzi wake hasa katika masuala ya upimaji wa VVU na ushauri nasaha, athari za uraibu wa dawa za kulevya, masuala ya kisaikolojia na magonjwa yasiyoambukiza.

"Novemba mwaka jana, Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, alizindua kituo baada ya kukamilika kwa ujenzi," anasema.

Anasema, kituo hicho kina umuhimu mkubwa katika jamii, hasa kutokana na kukumbwa na matatizo mengi yakiwamo mafarakano ya ndoa, kifamilia, misongo ya mawazo kutokana na ukosefu wa vipato toshelezi, ajira na mengine mengi yaliyo ndani ya jamii.

Mratibu wa kituo hicho, Rufina Khumbe, anasema huduma zinatolewa kwa kufuata watu sehemu mbalimbali na wengine kufika kituoni kuhudumiwa, wakiwamo waathirika wa majanga kama moto.

**ELIMU YA MAJANGA**

Mwanasaikolojia kutoka kituo hicho Dk. Zainabu Rashid anasema wanatoa elimu juu ya kujikinga na majanga mbalimbali ikiwa ni pamoja na moto, mafuriko na mikakati ya kuyakubali.

"Jamii yetu haina uelewa juu ya umuhimu wa huduma ya ushauri na msaada wa kisaikolojia kama tiba ya namna ya kupata suluhu ya matatizo yao kwa kuzungumza na wataalamu," anasema Dk. Zainabu.

Anasema, jamii haiamini katika ushauri pekee na kwamba wapo kwa ajili kuondoa dhana hiyo, majanga yanapotokea watu wafahamu jinsi ya kujiokoa na hata kuendelea kuishi baada ya matatizo kumalizika.

Anataja kazi iliyofanyika ya kutoa elimu kwenye soko la Mchikichini jijini Dar es Salaam, baada ya wafanyabiashara kuunguliwa bidhaa zao

"Baada ya kuwapa elimu, ushauri na msaada wa kisaikolojia, waathirika wa janga hilo la moto, waliridhika na kushukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwatambua na kuwaweka katika kundi maalum," anasema.




Mkuu wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Dk. Joyce Nyoni akiwa pamoja na wafanyakazi wa kituo hicho. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

> "Hatuishii hapo tu bali pia kwa wanaofanyakazi na jamii, kwa upande wa msaada wa kisaikolojia tunamrudisha mtu katika hali ambayo anaweza kuwa na manufaa katika jamii.



Mkuu wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Dk. Joyce Nyoni katika mahojiano.

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Uganda yafurahia, yaizawadia Siku Kiswahili Duniani waraka maalum

SERIKALI ya Uganda imetoa tangazo la kuratibisha ufundishaji wa Kiswahili kama somo la lazima shule za msingi na sekondari, kama mkakati wa kukuza matumizi ya lugha hiyo kitaifa.

Ni hatua itakayopendezesha Siku ya Kiswahili Duniani ambayo hapa nchini, kitaifa imefanyika Zanzibar pamoja na maadhimisho ya Sabasaba ambayo Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO) lilichagua kuwa ndiyo siku rasmi ya kukienzi na kukitafakari Kiswahili.

Ni hatua ambayo imewafurahisha wadau wa lugha hiyo nchini Uganda, wakiahidi 'kazi iendelee.'

Wachambuzi nchini Uganda wanaozungumza na vyombo vya habari vya kimataifa wanasema kuwa awali serikali ya Uganda ilisema lugha hiyo haiwezi kufundishwa shuleni kwani hakuna walimu wa kutosha kwa jukumu hilo, hali ambayo sasa imebadilika. Vyuo vikuu nchini humo vimeongeza walimu wengi wa lugha hiyo katika miaka 10 iliyopita na kuanza kufundisha somo hilo shuleni hakutahitaji kutafuta au kuajiri walimu kutoka nchi za jirani. Ni hatua ya kubadilisha kiasi fulani hulka nchini humo, kutumia lugha moja kuunganisha watu.

Licha ya kuwa hakuna hatua rasmi katika nchi nyingine za jirani kwa suala hilo, wachambuzi wanaona kuwa kuna uwezekano mfano huo wa Uganda kuigwa na mataifa jirani kwani zipo faida za kuingia katika mkakati wa kufundisha Kiswahili kwenye shule zote.

Faida hizo zinawezekana pia kuangaliwa nchini Malawi au DRC ambako Kiswahili si kigeni, na kunaweza kutoa hamasa kubwa kuunganisha wananchi kwa kukwepa lugha za kikabila zinazoshindana.

Hii imekuwa sababu mojawapo ya Kiswahili kukua kwa haraka na kuwa na ushindani kiasi fulani na Kiingereza kama lugha rasmi nchini Kenya. Sababu ni kuwa viongozi walikuwa wanatumia Kiingereza katika mikutano, na endapo hawakukitumia katika hadhara za umma, mara nyingi waliongea lugha ya kikabila ya eneo husika.

Mwelekeo huo wa kutumia lugha za kikabila katika mikutano ya hadhara unaonekana kuchangia kuyumbisha umoja, kwani kila lugha ina mambo yake na miiko yake iliyojengeka kihistoria.

Inawezekana Malawi ikawa na ugumu fulani kuanza kufundisha Kiswahili ili kiwe sehemu ya mkakati wa kuunganisha raia wake kitamaduni na hatimaye kisiasa. Kuna mgawanyiko wa jadi kati ya maeneo au majimbo ya kaskazini, kati na kusini, kama ilivyo kwa upande wa Msumbiji, ambako pia Kiswahili hakina wadau wenye nguvu.



Wanafunzi nchini Uganda wanatarajia kufundishwa Kiswahili kuanzia shule za msingi hadi taasisi za elimu ya juu. **PICHA: MTANDAO**

Kimsingi kina umuhimu kwani ilikuwa sehemu ya harakati za ukombozi, ila ukoloni ulipandikiza hisia kuwa ni lugha ya wafanya biashara ya utumwa na fikra hiyo iliendelea kujikita katika hisia za watu hata baada ya vita ya ukombozi kwa kukihusisha na utumwa.

Ugumu huo kimsingi haupo kwa upande wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo ambako Kiswahili kinatumika katika eneo la mashariki zaidi. Migawanyiko inayozusha vita imepungua ukilinganisha na miongo iliyopita, kwani maeneo mengine wanasiasa wake wamejikita katika makundi ya vyama yenye 'hesabu' tofauti za kushirikiana na kiongozi aliyepo au chama tawala, siyo kuanzisha makundi ya kivita kulazimisha wanachotaka kifanyike. Bado kuna angalau kundi moja lenye silaha, Mai Mai, ambalo lina mizizi ndani ya Congo, si wahamiaji au wakazi wa mashariki; utii wao kitaifa na undani wa uzalendo una mashaka.

Unaweza kusema kuwa kinacholeta msukumo hivi sasa wa kutumia lugha ya Kiswahili ni 'utandawazi kikanda,' ambako nchi zinahusiana kibiashara, kuanzia DRC hadi Kenya na hata Somalia au Sudan Kusini.

Kama mahusiano hayo si ya kampuni kubwa zinazoagiza vifaa au kuelekeza bidhaa kwa mtiririko wa kibiashara wa kimataifa, hivyo zitumie Kiingereza, wanaohitaji kusafiri hapa na pale, au kutafuta washirika, inasaidia wakiwa wanamudu Kiswahili.

Isitoshe changamoto ya kuhitaji kutumia lugha ya kikabila au Kiingereza, kwingineko Kifaransa, inakutana na hitaji la sasa la kutaka mawasiliano yawe ya 'Kiafrika zaidi.' Isitoshe kuna mashindano ya chinichini kati ya lugha za jadi zinazoshindana na lugha ya kigeni ya eneo fulani, iwe ni Kiingereza huko Malawi au Uganda au Kifaransa kwa upande wa DRC, Burundi na Rwanda.

Nchini Rwanda yako mabadiliko ya kutumia Kiingereza badala ya Kifaransa kama lugha rasmi ya kigeni kutokana na kuhusika kwa Ufaransa kuleta utawala wa siasa kali ulioua halaiki ya watu takribani 800,000 mwaka 1994. Kwa upande mwingine kuna lugha moja ya kikabila na pia kitaifa inayowaunganisha ya Kinyarwanda, kama ilivyo Burundi hivyo matatizo yao hayana upana wa lugha kusaidia kuyatatua ila siasa, sera.

Lakini kwa upande mwingine hata Rwanda na Burundi wanaweza kufaidika kwa kubadilisha mwelekeo wa lugha, angalau kupandikiza lugha nyingine kwani hata wao watakuwa wanakutana na wafanyabiashara kutoka ukanda wa Afrika Mashariki ambako ni wanachama.

> Suala hapa ni kuwa lugha za kikabila haziwezi kutenganishwa na hisia za upekee wa makabila hayo, na kila upekee una chembe ya ubaguzi kwa anayeongea lugha nyingine ya kikabila.

Hivi sasa wengi wanatumia Kiingereza kwani Kifaransa hakifahamiki huku, lakini Burundi inaongea Kiswahili kwa urahisi zaidi. Halafu ukiangalia televisheni zinazotumia lugha hizo, unakuta kuna ukaribu zaidi wa Kirundi na Kiswahili kuliko Kiganda, ambacho hakina mchango huo kwa uwazi.

Suala hapa ni kuwa lugha za kikabila haziwezi kutenganishwa na hisia za upekee wa makabila hayo, na kila upekee una chembe ya ubaguzi kwa anayeongea lugha nyingine ya kikabila na siyo ile.

Ni kanuni ya kitamaduni kuwa nikiongea kwa mfano Kizaramo naweza kumbagua Mkwere, ila siwezi kumbagua Mnyakyusa kwa kuongea Kiingereza, kwani ubaguzi huo hasa utakuwa ni wa kisomi na siyo wa kikabila, wakati kumbagua mtu kwa kutumia Kiswahili ni ishara ya kujivunia utaifa wenye mchongo wa lugha hiyo.

Rwanda iking'ang'ania Kinyarwanda na Kiingereza itaondoa ukabila kwa sera na siasa, huku utamaduni wa lugha ukichochea ukabila kutokana na nahau, hisia, misemo na vielelezo vya kujitofautisha kitamaduni ilivyo navyo.

Kama alivyosema Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere mwaka 1995, 'hii si sheria ya Mwalimu Nyerere, ni sheria ya historia kukausha ukabila kunahitaji lugha pana, zaidi ya kabila, na isiwe ni lugha ya mkoloni wa jadi, au mkoloni mbadala. Ndicho Uganda inachoona kinafaa na sasa inakifuata.

# Majeruhi kuuliwa, kuporwa, maiti kupekuliwa

INATOKA UK.11

magari ambao umekomaa, hivyo si suala la kupuuzwa tena.

Kikosi cha Usalama Barabarani kinaweza kujiaminisha kuwa kupungua kwa ajili kutamaliza tatizo hilo, lakini ukweli ni kwamba lazima maradhi hayo yapatiwe tiba maana inawezekana hata wakatumia mbinu nyingine ili kusababisha ajali na kuwaibia majeruhi au kuiba shehena.

### UFUMBUZI NA USHAURI

Hassan Mchanjama, Mwenyekiti wa Chama cha Kuwatetea Abiria (CHAKUA), anasema wizi kwenye ajali si jambo geni lakini suala hilo halijapewa uzito wa kutosha kulikomesha.

"Ni kawaida kusikia majeruhi wamenyongwa na mali zao zimeibwa lakini mbona hakuna sheria zinazotungwa kudhibiti hali hiyo? Tunahitaji sheria sasa." Anasema.

"Inakuwaje watu wanaowapekua majeruhi, wanawaumiza hata kuwaua, wanaiba kila kitu na miili inaporwa vitu vingi, lakini haijasikika kama kuna msako umefanyika na watuhumiwa kushtakiwa mahakamani kwenye eneo mkasa ulikotokea? Anahoji Mchanjama.

Anasema suala ambalo lingemaliza tatizo ni kuweka kamera zinazorekodi matukio kwenye barabara kuu kwa kuangalia pia sehemu ambazo zimekuwa sugu na kusababisha ajali mara kwa mara.



Magari madogo yanapopata ajali licha ya wizi na uporaji wa mali za abiria, wengine hunyongwa huku vifaa kama taa, betri na vioo vikiibwa pia. **PICHA MTANDAO**

Anaamini kuwa iwapo kutakuwa na kamera za kurekodi matukio hayo, ufuatiliaji unaweza kufanyika na hali hiyo ikadhibitiwa kuliko kuacha ibaki kama ilivyo, kwa vile wahalifu hawana cha kuogopa.

"Tunatakiwa pia kulizungumzia sana suala hili. Tusikae kimya na ikibidi kuwa wabunifu zaidi wakati wa wiki ya usalama barabarani hata kwenye uzinduzi wa barabara na miradi ya maendeleo kama hospitali ni lazima tulikemee hili." Anasema.

Anawataka viongozi wa dini wasiachwe nyuma wazungumzie wizi huo unaofanywa kwenye matukio ya ajali na kwamba vijana au wahusika hao hata kama hawaendi kwenye nyumba za ibada lakini jambo linapokemewa ni lazima watapata taarifa.

Kadhalika, Mchanjama analitaka bunge kuandaa sheria kupambana uhalifu huo ambao umejikiti kila mahali ajali zinapotokea, polisi nao wachunguze, wawashtaki watuhumiwa ili kudhibiti uhalifu huo unaoangamiza maisha, kuharibu mali na kusababisha umaskini.

### ATHARI KWA ABIRIA

Mchanjama anakumbusha kuwa wasafiri wanapoibiwa kila kitu inakuwa vigumu kuwasaidia maana simu ambazo zingefanikisha mawasiliano zimeporwa na kusababisha kukosekana taarifa za kuwapata jamaa zao ambao wangewapa msaada.

"Kadhalika wizi huo unachukua vitambulisho na nyaraka muhimu za utambulisho na kusababisha majeruhi walio taabani wachelewe kupata msaada wa jamaa zao na hata miili itambulike. Hili linawaathiri zaidi abiria ambao hawakutumia usafiri wa mabasi au magari mengine yaliyokuwa na safari rasmi," anaongeza.

Anasema abiria wanaopewa lifti, au wanaotumia pikipiki au wenye haraka wanaodandia magari wanaweza kuwa waathirika iwapo ajali itatokea na mali zao kuporwa, ikilinganishwa na waliotumia mabasi ambao taarifa zao zinaandikwa na nakala kupatikana ofisini.

Kadhalika kuua watu waliojeruhiwa ili kuwaibia ni unyama na ukatili sawa na hatia ya kuua kwa kukusudia ambayo ingempeleka mahakamani mshitakiwa na iwapo angepatikana na hatia hata naye angehukumiwa kifo.

Anasema zinapokosekana taarifa za wasafiri wakati mwingine miili yao huzikwa na serikali kwa maelezo kuwa hawakuwa na ndugu lakini ukweli ni kwamba hakuna Mtanzania ambaye hana ndugu au asiyefahamika.

Anakumbusha kuwa kila mmoja ana kitambulisho cha taifa, cha kura au leseni lakini hata wanafunzi wana vitambulisho na ikitokea wapo abiria watoto wanasafiri na jamaa, wazazi au walezi wao.

## WANENAVYO MALENGA

### MWANADAMU NAMUACHA

Mwanadamu namuacha, nachake hichokichaa,
Hivinasafishakucha, tumboni ninayo njaa,
Nasubiria kukicha, nifanye yanayofaa,
Mwanadamu hatihati, mwamini Mungu pekee.

Usinirushie vocha, nisije zuabalaa,
Mjadala ninakacha, nisije nikachakaa,
Sumu alikwishaacha, iwe ze kunivagaa,
Mwanadamuhatihati, mwamini Mungupekee.

Kirusi UKIMWI kocha, madhara yake balaa,
Na hicho kila kukicha, kivingine chatambaa,
Ukitege kwenye bucha, chenyewe kinasambaa,
Mwanadamu hatihati, mwamini Mungu pekee.

Namuona wangu pacha, kutoka najiandaa,
Zipu waziameacha, watu wanamshangaa,
Badala ya kumficha, picha ndiyo zasambaa,
Mwanadamu hatihati, mwamini Mungu pekee.

Macho ninayafikicha, nione anapokaa,
Nyumba yake nipakacha, imejengwa kwa mkaa,
Mbona kuunguza picha, bila mafuta ya taa?
Mwanadamu hatihati, mwamini Mungu pekee.

Kiburi change naficha, nisijezua balaa,
Ninakwenda Kiraracha, kwenye baridi kukaa,
Hasira zitapoacha, nitazidi kushangaa,
Mwanadamu hatihati, mwamini Mungu pekee.

Mipango kila kukicha, wewe uweze kupaa,
Hata madawa pekecha, pazuri uwezekaa,
Mungu nawangu uticha, wala sitalala njaa,
Mwanadamu hatihati, mwamini Mungu pekee.

Utukufualiacha, akaja kwetu kukaa,
Kweli yake hakuficha, hata walipokataa,
Na kuonya hakuacha, watu waache tamaa,
Mwanadamu hatihati, mwamini Mungu pekee.

Kukung'ong'a hataacha, hata kama wamfaa,
Mema kwako ataficha, ubaki unashangaa,
Aweza kutoakucha, ubaki unatambaa,
Mwanadamu hatihati, mwaminiMungupekee.

Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)
lwagha@gmail.com 0767223602

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

### VITA NA IENDELEE

Kufa kweli kufaana, na vita iendelee,
Wengine wanauana, acha wao wapotee,
Wengine ndio wavuna, silaha wazipokee,
Mahitaji ya dunia, mambo ni mchanganyiko.

Matamshi yapingana, hebu acha yatokee,
Wengineo wanaona, vita na iendelee,
Wengine wabishisana, wanataka ipotee,
Mahitaji ya dunia, mambo ni mchanganyiko.

DR Congo twaona, acha watu wachochee,
Watu wazidipigana, na maisha yapotee,
Huku wengine kuvuna, madini kuendelee,
Mahitaji ya dunia, mambo ni mchanganyiko.

Amani wengi waona, itafanya walegee,
Sababu vita wanona, wabakiwa chekelee,
Silaha wauziana, pesa wajiongezee,
Mahitaji ya dunia, mambo ni mchanganyiko.

Hata magonjwa twaona, yaache yaendelee,
Kama wote watapona, hizi kazi zipotee?
Dawa tunauziana, lazima ziendelee,
Mahitaji ya dunia, mambo ni mchanganyiko.

Muuza ndizi twaona, ata kazi sipotee,
Nunua zote hapana, ni bora zimuozee,
Mzidi kuuziana, maisha yaendelee,
Mahitaji ya dunia, mambo ni mchanganyiko.

Mpenyo akiuona, mlipuko utokee,
Itabaki kukutana, na kazi iendelee,
Wazidi kuvurugana, na kazi zisipotee,
Mahitaji ya dunia, mambo ni mchanganyiko.

Endelea kupigana, hasara na zitokee,
Huku nyie mwauana, wengine wachekelee,
Faida wanaziona, wabakiwa zipokee,
Mahitaji ya dunia, mambo ni mchanganyiko.

Ulaya wanapigana, shida kwetu zitokee,
Bei zavitu twaona, wengine wachekelee,
Wanavuna wanavuna, faida iendelee,
Mahitaji ya dunia, mambo ni mchanganyiko.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**





# H'shauri zapewa 'kibano' taarifa za miradi viporo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imeagiza Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa halmashauri zinaandaa taarifa ya miradi viporo iliyopo katika maeneo yao na kubainisha sababu za kuwapo miradi hiyo.

Naibu Katibu Mkuu wa ofisi hiyo, Ramadhani Kailima alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akifunga kikao kazi cha makatibu tawala wasaidizi sehemu ya Mipango, Uratibu na Usimamizi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Maofisa Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji na Waweka Hazina wa Halmashauri kilichofanyika, jijini hapo.

Kailima alitaka taarifa ya miradi hiyo viporo iwasilishwe Ofisi ya Rais -TAMISEMI kabla ya Julai 25, mwaka huu.

Pia aliagiza sekretarieti hizo kuandaa taarifa ya mpango kazi wa mtiririko wa fedha na manunuzi kwa mwaka 2022/23 na kuwasilisha kabla ya Julai 20, mwaka huu.

Kailima alibainisha kuwa mikoa inatakiwa kukamilisha marekebisho yote ya bajeti ili kuingizwa katika mfumo wa matumizi na halmashauri zinazopokea fedha za hisani za kampuni kwa jamii zihakikishe fedha hizo zinaingizwa kwenye mipango ya bajeti za halmashauri husika.

Alisisitiza mikoa ifanye uchambuzi wa fedha za maendeleo zinazopelekwa katika miradi ya maendeleo kulingana na asilimia 40 kwa 60 za uchangiaji kutokana na kuhakikisha fedha hizo zinatekeleza miradi ya maendeleo iliyopangwa na serikali.

"Nendeni mkahakiki maeneo ya utekelezaji wa miradi kabla ya fedha za miradi kutolewa ili kujiridhisha na maeneo hayo kutokuwa na migogoro ya umiliki wa ardhi," alisisitiza Kailima.

Alitaka Sekretarieti za Mikoa kuzisimamia halmashauri kuhakiki maeneo yatakayojengwa miradi ya maendeleo kama elimu na afya kupimwa na kupata hati miliki kisheria.



Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Dodoma, Pili Mbanga (kushoto), akimkabidhi fomu ya kugombea ujumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa, Lukanus Kayombo, jana katika ofisi za chama hicho jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Askofu atoa ushauri uhakika wa chakula

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Baptist Tanzania, Arnold Manase, ameishauri serikali kuzuia usafirishaji wa mazao nje ya nchi ili taifa liwe na uhakika wa akiba ya chakula wakati huu ambapo kuna tishio la kupanda kwa bei.

Ushauri huo aliutoa juzi jijini hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mambo mbalimbali ya kitaifa ikiwamo sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika mwezi ujao.

Alisema kuna kila sababu ya serikali kuzuia uuzaji wa mazao nje ya nchi na kuweka akiba ya kutosha ya chakula kutokana na upungufu mkubwa ulipo mwaka huu katika maeneo mengi nchini na nje ya nchi.

"Nimekuwa nikiuliza kwa wachungaji wangu katika maeneo mbalimbali kuhusu hali ya chakula katika maeneo yao na bei ya vyakula wananieleza kuwa bei zipo juu sana na Wakenya wanaenda hadi maeneo ya vijijini kununua mazao na Watanzania hakuna mtu mwenye akili hiyo hali hii inamaanisha kuwa tunaweza kuwa na njaa nchini wakati wenzetu wamenunua chakula chote kwa wakulima wetu vijijini."

"Unaweza kuona jinsi gani wafanyabiashara wa nchi jirani wanavyotumia juhudi kubwa kununua chakula cha kutosha na kukihifadhi kama sisi tutaishiwa chakula tutalazimika kununua kwa majirani tena kwa bei kubwa jambo ambalo litasababisha kuwapo kwa tishio la njaa," alisisitiza Askofu.

Alisema ni ukweli usiopingika kama nchi haitakuwa na chakula cha kutosha uchumi hauwezi kukua na uzalishaji utakuwa wa kusuasua katika jamii.

"Serikali inabidi sasa kuangalia namna bora ya kuyatumia maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji ili kutumia njia ya haraka kukabili uhaba wa chakula ulipo hivi sasa katika nchi nyingi."

"Sisi ndiyo tumekuwa tegemeo kubwa kwa nchi nyingi zinazotuzunguka kama Kenya, Sudan, Uganda, Somalia kuwauzia chakula, lakini na sisi sidhani kama tunayo akiba ya kutosha hivyo ni jukumu la serikali pamoja na sisi viongozi wa dini kutoa elimu kwa wananchi wetu kuhifadhi chakula walichonacho," alisema.

Akizungumzia bajeti kuu iliyopitishwa na Bunge hivi karibuni, alisema kiasi ambacho kimetengwa kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 kinapaswa kupelekwa kama kilivyotengwa ili kugusa moja kwa moja maisha ya wananchi.

Alihimiza Watanzania kujitokeza kwa wingi kushiriki sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika mwezi ujao ili kuiwezesha serikali kupata takwimu sahihi kwa ajili ya kupanga mipango ya maendeleo.

# 'Mkapa Fellow' yasaidia huduma rafiki kwa vijana

**Na Augusta Njoji,** CHEMBA

TAASISI ya Benjamin Mkapa (BMF), kupitia mradi wa 'Mkapa Fellow' awamu ya tatu, imetajwa kusaidia kuondoa vikwazo vya upatikanaji wa huduma rafiki kwa vijana Wilaya ya Chemba.

Miongoni mwa vikwazo hivyo ni pamoja na kukosekana kwa elimu ya uzazi wa mpango, kujikinga na Virusi vya Ukimwi, dawa za kulevya na ukatili wa kijinsia kwa vijana.

Mganga Mkuu wa wilaya hiyo, Dk. Marko Mgonja, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mradi huo unaofadhiliwa na Serikali ya Ireland kupitia mfuko wa Irish Aid ikiwa ni kuelekea jukwaa la kumbukizi ya pili ya aliyoyafanya na kuacha alama mwasisi wa taasisi hiyo, Hayati Rais Benjamin Mkapa, litakalofanyika Julai 13 - 14 visiwani Zanzibar.

Alisema kupitia mradi huo halmashauri imeongeza idadi ya vituo vinavyotoa huduma rafiki kwa vijana kutoka 10 hadi 35 na wamekuwa wakielimisha masuala ya uzazi wa mpango na matumizi ya kondomu ili kujiepusha na maambukizi ya VVU.

"Katika kipindi cha Desemba-Februari 2022 ni vijana 316 tu walipata huduma za masuala ya uzazi, lakini katika kipindi cha Machi hadi Mei 2022, jumla ya vijana 1,135 (359%) walipata huduma hizo," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa Miradi Mwandamizi wa Taasisi hiyo, Daudi Ole Mkopi, alisema taasisi hiyo inafanya kazi ya kuimarisha mifumo ya sekta ya afya kwa jamii.

"Katika kuhakikisha jamii hususani vijana wanapata elimu sahihi na kutafuta huduma hizo katika vituo vya kutolea huduma kwa wakati, BMF imekuwa ikifanya kazi kwa ukaribu na vijana kundi balehe ili kufikisha ujumbe katika jamii wanayoishi," alisema.

Alisema mradi huo umesaidia hadi sasa vijana wameunda makundi 30 yenye wanachama 395 na wanakutana mara moja kila wiki kujadili masuala ya afya.

"Hawa waelimishaji rika wameweza kuwafikia vijana wenzao wapato 2,483 na kutoa elimu mbalimbali kama vile matumizi sahihi ya kondomu, elimu ya afya ya uzazi, magonjwa ya ngono, ukatili wa kijinsia, elimu ya lishe na dawa za kulevya pindi wanapotembelea kaya na wenye mikutano ya hadhara," alisema.

Alisema katika kukabiliana na vikwazo vya kiuchumi vinavyosababisha vijana kujiingiza kwenye tabia hatarishi, vijana hao wamebuni miradi ya maendeleo na ujasiriamali.

Alisema ndani ya miezi mitatu vikundi 18 vimeanzisha shughuli za ufugaji wa kuku, sungura, nguruwe, kilimo cha mboga, alizeti na ushonaji wa nguo.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii wa wilaya hiyo, Verdiana Joseph, alisema mradi huo umefanikiwa kuwaondoa vijana kwenye makundi hatarishi ikiwamo kundi la vijana lililojiita Maronjo ambalo lilikuwa linajihusisha na ubakaji.

"Pamoja na kukamatwa, kwasasa vijana ambao ni miongoni mwa kundi hilo wameacha tabia hizo na sasa wanajishughulisha na miradi ya kilimo cha mboga na ufugaji wa kuku," alisema.





# Serikali yaagiza kilio cha wakulima vipimo kisikilizwe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya, imeutaka Wakala wa Vipimo nchini (WMA), kushughulikia malalamiko ya wakulima ikiwamo kukomesha vipimo visivyoruhusiwa kwa mujibu wa sheria ili kuepuka wakulima kunyonywa na wanunuzi wa mazao.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo ndani ya mkoa huo ikiwamo ukusanyaji wa mapato. Homera alisema katika mkoa huo kuna baadhi ya wanunuzi wanawanyonya wakulima kwa kununua mazao yao wakitumia vipimo visivyoruhusiwa kama vile ujazo wa lumbesa na kushindilia mazao kwenye mifuko wakati wa kujaza.

Alisema vipimo hivyo vinaendelea kutumika katika ununuzi wa mazao kama mpunga na viazi jambo ambalo linawasababishia wakulima hasara ama kupata faida ndogo kuliko nguvu wanazotumia kwenye uzalishaji.

Alisema vipimo hivyo vimekuwa vikiendelea kutumika kutokana na maofisa wa Wakala wa Vipimo mkoani humo kutotekeleza majukumu yao ipasavyo na ili kukomesha vipimo hivyo, serikali itaanza kuwachukulia hatua maofisa hao.

"Kwa sasa hivi vipimo vinatumika sana kwa wakulima wetu wa mpunga Mbarali, Kyela na Chunya pamoja na kwa wakulima wa viazi katika wilaya za Mbeya na Rungwe, sasa nawaagiza maofisa wa wakala wa vipimo kushughulikia jambo hili haraka sana," alisema Homera.

Alisema ununuzi wa mazao kwa kutumia vipimo hivyo hauwaumizi wakulima pekee bali hata serikali inakosa mapato yake halali ambayo inatakiwa kukusanya kwenye biashara hiyo.

Baadhi ya wakulima katika mkoa huo waliiomba serikali kuwasaidia kudhibiti vipimo hivyo wakieleza kuwa vimekuwa vikitumika kuwanyonya.

Mmoja wa wakulima hao, Joshua Sanga, anayelima viazi katika Kata ya Ntokela, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, alisema wanatumia gharama kubwa kuzalisha mazao yao, lakini vipimo vinawaumiza.

Alisema kwenye biashara ya viazi wanunuzi wanaenda na mifuko ambayo ujazo wake haujulikani na baadhi yao wanatumia mifuko midogo maarufu kwa jina la vipeto ambavyo huwa wanadai vikiwa viwili ni sawa na mfuko mmoja wa kilo 100.

"Hivi vipeto tumejaribisha hivi karibuni na tulibaini kuwa vikiwa viwili ni zaidi ya kilo 120, sasa vipimo hivi ni vizuri vikaondolewa na serikali itoe maelekezo ya vipimo sahihi vya kutumia ili tusiendelee kunyonywa," alisema Sanga.

Mwaka huu, alisema wamenunua mbolea kwa bei kubwa ambayo ilisababisha gharama za uzalishaji kuwa kubwa na wakiuza mazao yao kwa kutumia vipimo hivyo kuna hatari ya kupata hasara zaidi ya mara mbili.

Hivi karibuni wakulima wa mpunga katika Skimu ya Matebete wilayani Mbarali, waliiomba serikali iwalazimishe wanunuzi wa mazao yao kutumia mizani kununua badala ya kukadiria mifuko.

Mwaka 2021, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliagiza Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na viongozi wa Mkoa wa Mbeya kukomesha vipimo vya ujazo mkubwa kwenye ununuzi wa mazao ya wakulima, lakini mpaka sasa vipimo hivyo vinaendelea kutumika.



Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi Ulrich Matei, akizungumza na madereva wa malori ya mizigo katika maegesho yaliyoko Maghorofani jijini humo, aliongoza shughuli ya ukaguzi wa mifumo ya magari hayo mwishoni mwa wiki ili kupunguza ajali za barabarani. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Zaidi ya makada 1,000 CCM waomba uongozi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya makada 1,080 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani hapa, wamejitokeza kuomba ridhaa ya chama hicho kuwania nafasi mbalimbali za uongozi.

Katibu wa CCM Mkoa wa Mbeya, Mwalimu Akwilombe, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kuwa wanachama waliojitokeza kuwania nafasi hizo ni wengi kutokana na fomu hizo kutolewa bila gharama.

Alisema fomu hizo zimekuwa zikichukuliwa na makada hao kwenye ofisi za chama katika wilaya zote na ofisi ya chama mkoa na jumuiya zake zote.

Alisema uchukuaji wa fomu ulifunguliwa Julai 2, mwaka huu na kutakiwa kufungwa Julai 10, na nafasi zinazowaniwa ni za kuanzia ngazi ya wilaya mpaka taifa.

"Zoezi hili tutafunga Julai 10 saa 10:00 jioni, lakini mpaka sasa mkoa mzima wanachama waliochukua fomu wapo zaidi ya 1,080 na naamini mpaka kufika siku ya mwisho watakuwa wameongezeka zaidi," alisema Akwilombe.

Aliwataka wanachama wa chama hicho kuendelea kuzingatia sheria na kanuni za uchaguzi ili kuepuka kuenguliwa kwenye kinyang'anyiro hicho kwa mujibu wa sheria za chama.

Alisema nafasi ambazo wanachama wamejitokeza zaidi kuziomba ni za ujumbe wa mkutano mkuu wa chama hicho ambao nafasi 15 zinatolewa kwa makada wa Tanzania Bara na vingine 15 kwa makada wa Tanzania Visiwani.

Alisema chama hicho kinafanya uchaguzi huo ili kuimarisha uongozi wa kidemokrasia na kusisitiza kuwa ndicho kinachoongoza kwa kufuata demokrasia nchini.

# Baadhi wazazi wadaiwa kushawishi watoto wao wasifanye vizuri shuleni

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

BAADHI ya wanawake katika Kijiji cha Ilasilo, Kata ya Garula wilayani Songwe, wanadaiwa kuwa vinara wa kuwashawishi watoto wao wa kike kutofanya vizuri kwenye mitihani ili wawaozeshe na kujipatia mali jambo ambalo linahesabika kama ni ukatili wa kijinsia.

Diwani wa Viti Maalumu Kata ya Garula, Pascalina Shitundu, aliyasema hayo juzi wakati wa mkutano wa hadhara ambao uliandaliwa na Shirika la Maendeleo la ADP Mbozi, katika Kijiji cha Ilasilo.

Shirika hilo linahusika na mradi wa uhakika wa chakula katika familia na kudai wanawake wamekuwa wakikiuka haki za msingi za watoto kwa kuchochea ndoa za utotoni na kata ya Garula ni miongoni mwa maeneo ambayo mradi unatekelezwa.

Alisema tabia hiyo inamsikitisha kwa sababu wanawake wenzake ambao walitakiwa wawe wanapambana na ukatili dhidi ya watoto, lakini wao wamegeuka kuwa vinara wa kushiriki vitendo hivyo.

"Ninasikitika kwamba wanawake wenzangu ndio mnawahamasisha watoto wasifanye vizuri kwenye mitihani ili muwaozeshe, sasa unamwozesha mtoto mdogo ili akafanye nini kwenye ndoa? Nawaombeni wanawake wenzangu tuwasaidie watoto wetu," alisema Pascalina.

Mwakilishi wa Shirika la ADP Mbozi, Jackline Sanga, alisema wanawake wamekuwa wakikabiliana na matatizo mbalimbali yakiwamo ya ukatili pamoja na mabadiliko ya tabia nchi ambayo yanasumbua dunia kwa sasa.

Alisema watoto wa kike wanaanza kupata matatizo ya ukatili wa kijinsia kuanzia kwenye familia, shuleni na kwenye ndoa na kutaka kila mdau kushiriki kwenye ulinzi huo.

Aliwataka wananchi kuwasaidia watoto wa kike kwenye mambo mbalimbali ikiwamo kupata nafasi za uongozi ili kuwa na usawa kwenye jamii.

Kaimu Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Songwe, Wambi Mwalukisi, alisema hivi karibuni halmashauri hiyo iliwaokoa watoto watatu waliokuwa wanasafirishwa kwenda kutumikishwa kwenye kazi za ndani.

Alisema baadhi ya watoto hao waliokuwa wamefaulu darasa la saba na kutakiwa kujiunga na kidato cha kwanza, lakini wazazi wao wakaamua kuwapeleka kwenye vibarua.

Alisema vikundi vya makuzi na malezi vilivyoanzishwa kwenye jamii vinasaidia kutoa taarifa za ukatili dhidi ya watoto na wanawake kwenye jamii.





## Mke wa Rais Mwinyi awaasa watoto uangalifu siku za sikukuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariamu Mwinyi amewataka watoto wanaolelewa katika vituo mbalimbali kuwa makini na waangalifu wakati wanapokwenda na kurudi katika viwanja vya sikukuu, ili kuepukana na changamoto mbalimbali zinazoweza kuwakuta.

Mama Mariamu ambaye ni Mwenyekiti wa Taasisi ya 'Zanzibar Maisha Bora Foundation (ZMBF)' ametoa wito huo kwa nyakati tofauti alipotembea vituo mbalimbali vinavyotunza na kulea watoto na kuwakabidhi zawadi.

Katika hafla hiyo mama Mariamu aliwakilishwa na Mtendaji Mkuu wa ZMBF, Mwanaidi Mohamed Ali, alitembelea vituo vya ZASO Children Home kiliopo Founi Mambosasa, Kituo cha SOS pamoja na Kituo cha Kulelea watoto Mazizini, Mkoa Mjini Magharibi.

Alisema kuna umuhimu mkubwa kwa watoto hao kujilinda wakati wote wanapokwenda na kurudi kwenye viwanja vya sikukuu, huku akiwataka watoto wenye umri mkubwa kubeba dhima ya uangalizi kwa wale wenye umri mdogo ili kuwa salama.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee, Abdalla Saleh Omar, aliwataka watoto hao kufuata maelekezo wanayopewa na walezi wao, na kujikinga na vishawishi vyote ili kufanikiwa.

Aliwakumbusha watoto hao wajibu walionao wa kuongeza bidii katika masomo yao, akibainisha hatua hiyo itawawezesha kufikia mafanikio makubwa katika siku za usoni.

Alisema, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, awamu ya nane itaendelea kuwahudumia kikamilifu watoto wote nchini.

Mkurugenzi huyo alisema kipindi hicho cha sikukuu ni wakati wa furaha kwa watoto wote, akawataka kuthamini viongozi wa Maisha Bora Foundation, chini ya uongozi wa Mama Mariamu kwa kufika vituoni humo na kutoa mkono wa Idd el Hajj.

# Mwinyi awataka Wazanzibar kuthamini amani ya nchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesisitiza amani na utulivu wa nchi ili wananchi kuendelea kubaki salama.

Aliyasema hayo jana mjini hapo katika hafla ya dua ya kitaifa pamoja na chakula cha mchana kwa ajili ya watoto yatima kilichoandaliwa na taasisi ya kusaidia watoto yatima (Nuru Fondation).

Alisema zipo nchi ambazo zimeshindwa kuitumia rasilimali ya Mwenyezi Mungu ya amani, utulivu na usalama na zinaendelea kuwa na machafuko ya vita, na kwamba ni vyema Wazanzibar wakaithamini rasilimali hiyo.

Alisema kuwa dini zote zinahimiza kuwahudumia, kuwatunza, kuwathamini na kuwalea malezi mema watoto yatima.

Aliipongeza taasisi hiyo kwa hafla hiyo ambayo inaendana na utekelezaji wa maamrisho ya dini ya kuwalea watoto hao na yanafadhila kubwa.

Aliwataka wazazi kutekeleza wajibu wa kuwalea watoto wote vizuri bila ya kuwanyanyapaa au kuwatenga watoto yatima.

"Lazima kuwajengea mazingira mazuri watoto yatima yatayowaondolea huzuni ya kuondokewa na wazazi wao," alisema Dk. Mwinyi.

Alisisitiza kuwa na upendo wa mayatima na kwa pamoja kusaidiana kuwatunza watoto hao.

Alisema zipo asasi zinazohudumia watoto yatima, lakini michango yao haionekani na kusema ni vyema kuwa na uratibu kwa taasisi hizo ili lengo lake lionekana na kuleta faida.

Naye Mwenyekiti wa taasisi hiyo ya Nuru, Zainab Kombo, alisema malezi ya watoto yatima yana changamoto nyingi na kusisitiza jamii kuwa na ushirikiano katika malezi ya watoto.

Aliiomba serikali kuratibu shughuli ya kusaidia watoto yatima kwa sababu bila ya kuratibu kuna hatari ya watu kutumia vibaya kuwalea watoto hao na kuwavunja moyo wenye nia njema ya kuwasaidia.

"Katika upendo Mungu huleta nuru na kusafisha nyoyo za waja, shughuli hii imetufunza kuwa watu wanaguswa na watoto yatima," alisema.

Katibu wa Mufti Zanzibar, Khalid Ali Mfaume, alisema watoto yatima wanahitaji kusaidiwa na kuitaka jamii kusimamia mali za watoto yatima.

Alisema wanaokula mali za yatima kwa dhuluma wanakula moto na watafufuliwa wakiwa wanafuka moshi siku ya kiama.

Pia alisema katika Mahakama za Kadhi kuna kesi ambazo zinashughulikiwa za watoto yatima kudhulumiwa mali zao baada ya wazazi wao kufariki.




Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban, akizungumza na waandishi wa habari nje ya ukumbi wa mkutano wa siku 3 wa mafunzo yanayowakutanisha watendaji na taasisi zinazojishughulisha na kazi za ubunifu, alipoufungua mkutano huo hoteli ya Verde mjini Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Bara la Afrika latakiwa kulinda kazi za wabunifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NCHI za Bara la Afrika zimetakiwa kutayarisha sera ambayo itasaidia kulinda kazi za wabunifu hatua ambayo itasaidia kuongeza kipato na kuinua uchumi.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, wakati akifungua mkutano wa siku tatu wa mafunzo yanayowakutanisha watendaji na taasisi zinazojishughulisha na kazi za ubunifu.

Alisema nchi za Afrika bado zipo nyuma katika ubunifu wa hatimiliki ya kazi mbalimbali zinazofanywa na wazalishaji na wakati mwingine kupotea bila ya kufanyiwa kazi.

Alifafanua kuwa sera ndiyo mwongozo ambao utawawezesha wabunifu wa hatimiliki kuibua changamoto zinazowakabili katika kazi zao kwa ajili ya kutambuliwa na kuingiza kipato kikubwa kiuchumi.

Alisema baadhi ya nchi duniani zimepiga hatua kubwa ya maendeleo kutokana na kazi za wabunifu kutambuliwa na kupata hatimiliki na kuinua hali ya kiuchumi.

"Wakati umefika kwa nchi za Bara la Afrika kuja na mikakati ya sera ya ubunifu wa hatimiliki ambayo itasaidia kuweka mwongozo unaofahamika katika kulinda kazi za ubunifu na hatimiliki," alisema.

Naye Mwakilishi wa Taasisi ya hatimiliki ya Kanda ya Afrika (ARIPO), Said Hamadi alisema lengo la mafunzo hayo ni kuangalia ubunifu katika kuchambua utafiti mbalimbali ili kulinda hatimili za wazalishaji wake.

"Zipo tafiti mbalimbali za ubunifu zinazotokana na wazalishaji wa viwanda, kilimo na ugunduzi wa dawa za kienyeji ambazo ni muhimu kutambuliwa kwake," alisema.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Wakala wa Biashara na Leseni (BRELA), Seka Kasera, alisema mafunzo hayo yametayarishwa kwa ajili ya kuwapatia wabunifu mbinu ambazo zitawawezesha kuongeza kasi ya uvumbuzi wa kazi zao na kuziingiza sokoni pamoja na kupata hatimiliki.

"Wapo wabunifu wengi wenye uwezo na kipaji cha kuibua kazi zao, lakini tatizo bado lipo katika kutambuliwa baada ya kufanyiwa kazi na hatimaye kupata hatimiliki," alisema.

Kwa upande wa serikali ya mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na mali kutoka Zanzibar, Mkurugenzi Mtendaji, Mariyam Mliwa, alisema kwa upande wa Visiwani mafunzo hayo ni muhimu kwa kuwa yatasaidia kuwaibua wabunifu na kusajili kazi zao kutambuliwa na kupata hatimiliki.

"Haya ni mafunzo muhimu ambayo lengo lake kubwa ni kuibua vipaji vya wabunifu mbalimbali katika kazi zao ambazo hatimaye zitawawezesha," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**JUDITH BENEDICT MERERE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3822-0046** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya **TERESA OF CALCUTA SECONDARY** mwaka 2012,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi taarifa **DAR/OST/RB/258135/2020**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GODWIN ROBERT SANDY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha kidato cha nne chenye index namba **S0388-0081** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **MARANGU** mwaka **2000,** yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa DAR/URA/RB/269029/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA. 91 YA MWAKA 2020**
**BAINA YA**
**HERMIT INTERNATIONAL COMPANY LIMITED......MDAI**
**DHIDI YA**

**1.JOSEPH MICHAEL BUNDARA**
**2. PAULINA JOSEPH EMANUEL**
**3. ABIUDI KASWAMILA—WADAIWA**

**KWA:**

**1.JOSEPH MICHAEL BUNDARA**
**2. PAULINA JOSEPH EMANUEL**
**3. ABIUDI KASWAMILA**

**POPOTE PALE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**
Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili Wewe binafsi,Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 25.07.2022 saa 3.00 asubuhi.Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANGALIZO:** -Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu,Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito,Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hiloi leo tarehe 08 ya Mwezi wa Julai,2022.

.......................................................
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA DODOMA**

## KUPOTEA KWA VYETI



**KEVIN RUGAIMUKAMU** anatangaza kupotelewa na vyeti vya chuo,cha **BACHELOR OF ARTS (ECONOMICS & STATISTICS)** chenye namba ya usajili **2007-04-05245** kilichotolewa na UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM mwaka 2010 na cheti cha chuo cha MASTERS OF ARTS chenye namba za usajili **2010-06-01489** kilichotolewa na UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM mwaka 2012, yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/URA/RB/273888/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



**KEVIN RUGAIMUKAMU** anatangaza kupotelewa na vyeti ,cha kidato cha nne chenye index namba **S0800-0105** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **LOYOLA mwaka 2004** na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0800-0607** kilichotolewa na baraza lamitihani kupitia shule ya secondary ya LOYOLA mwaka 2007,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **UD/RB/4666/2012**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MOROGORO**
**SHAURI LA RUFAA YA ARDHI 34 YA 2022**
**ILIYASA ALLY CHUI.........................................................MDAI**
**DHIDI YA**
**MOROGORO URBAN WATER SUPPLY AND SANITATION AUTHORORITY,**
**MOROGORO MUNICIPAL COUNCIL, NAB POWER SERVICES LTD.....WADAIWA**
**WITO WA MAHAKAMA**
**KWA: NAB POWER SERVICES LTD**

**WITO huu ni wakesi tajwa hapo juu,** ambayo imepangwa kutajwa tarehe 26/07/2022
saa 03:00 asubuhi mbele ya Mheshimiwa Jaji Chaba.
Unatakiwa kuhudhuria wewe binafsi au wakili au mtu yeyote aliyeidhinishwa kusimama kwa niaba yako napia unatakiwa kutoa maelezo yako siku hiyo na nakala zote za ushahidi utakazo tumia kwa shauri hili.

**Zingatia Kwamba** ,kutohudhuria siku ya kesi na kwa wakati uliotajwa hapo juu,Mahakama itaendelea kusikiliza shauri hili nakutoa maamuzi bila ya uwepo wako.

Imetolewa chini ya Muhuri wa Mhakama Kuu Kanda ya Morogoro leo siku ya tarehe 05/07/2022.

.......................................................
NAIBU MSAJILI MAHAKAMA KUU
MOROGORO

**Summons to appear (O.VR.20(1) of (CPC)**
**(Substituted Service)**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**MISCELLANEUS LAND CASE APPLICATION NO 47 OF 2022**
**THE REGISTERED TRUSTEES OF MITO YA BARAKA......PLAINTIFF**
**VERSUS**
**MOSES BARNABAS & OTHERS..................DEFENDANTS**

**TO: KEITH MUKAMI – DAR ES SALAAM**

**WHEREAS:** The above named **PLAINTIFF** has instituted the **SUIT** against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or agent duly authorized on **03th day of AUGUST 2022 at 09:00 AM** before **Hon. A. MSAFIRI. JUDGE (Chamber No. 32)** in the morning to answer the said **SUIT** and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of you **REPLAY.**
**TAKEN NOTICE** that, in default of your appearance on that day the suit will be heard and determined in your absence.
**GIVEN UNDER MY** hand and the seal of this Court, this **8th day of JULY, 2022.**

DEPUTY REGISTRAR

**Summons to appear (O.VR.20(1) of (CPC)**
**(Substituted Service)**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**MISCELLANEUS LAND CASE APPLICATION NO 47 OF 2022**
**THE REGISTERED TRUSTEES OF MITO YA BARAKA................PLAINTIFF**
**VERSUS**
**MOSES BARNABAS & OTHERS..................DEFENDANTS**

**TO: ANASTAZIA MUKAMI – DAR ES SALAAM**

**WHEREAS:** The above named **PLAINTIFF** has instituted the SUIT against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or agent duly authorized on **03th day of AUGUST 2022 at 09:00 AM** before **Hon. A. MSAFIRI. JUDGE (Chamber No. 32)** in the morning to answer the said **SUIT** and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of you **REPLAY.**
**TAKEN NOTICE** that, in default of your appearance on that day the suit will be heard and determined in your absence.
**GIVEN UNDER MY** hand and the seal of this Court, this **8th day of JULY, 2022.**

DEPUTY REGISTRAR

**Summons to appear ( O.VR.20(1) of (CPC)**
**(Substituted Service)**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**MISCELLANEUS LAND CASE APPLICATION NO 47 OF 2022**
**THE REGISTERED TRUSTEES OF MITO YA BARAKA ......PLAINTIFF**
**VERSUS**
**MOSES BARNABAS & OTHERS.................DEFENDANTS**

**TO:**
**BORA MUKAMI**
**DAR ES SALAAM**

**WHEREAS:** The Above Named **PLAINTIFF** has Instituted The **SUIT** against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or agent duly authorized on **03rd day of AUGUST 2022 at 09:00 am** before **hon. A. MSAFIRI..JUDGE (chamber no.32)** in the morning to answer the said suit and you are directed to produce on that day all documents upon which you intend to rely in support of **REPLAY.**
**TAKE NOTICE** That, in default of your appearance on that day the suit will be heard and determined in your absence.
**GIVEN UNDER MY** hand and the seal of this Court, this **8TH day of JULY 2022.**

DEPUTY REGISTRAR

**Summons to appear (O.VR.20 (1) of (CPC)**
**(Substituted Service)**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**MISCELLANEUS LAND CASE APPLICATION NO 47 OF 2022**
**THE REGISTERED TRUSTEES OF MITO YA BARAKA .......PLAINTIFF**
**VERSUS**
**MOSES BARNABAS & OTHERS..................DEFENDANTS**

**TO:**
**GALUS MUKAMI**

**WHEREAS:** The Above Named **PLAINTIFF** has Instituted The **SUIT** against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or agent duly authorized on **03rd day of AUGUST 2022 at 09:00 am** before **hon. A. MSAFIRI..JUDGE (chamber no.32)** in the morning to answer the said suit and you are directed to produce on that day all documents upon which you intend to rely in support of **REPLAY.**
**TAKE NOTICE** That, in default of your appearance on that day the suit will be heard and determined in your absence.
**GIVEN UNDER MY** hand and the seal of this Court, this **8TH day of JULY 2022.**

DEPUTY REGISTRAR

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**VASCO ELIAS BOKELLA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **TVS BLACK** yenye namba za usajili **MC 214 CRE,** chasis namba **MD625AF43L1H01376,** engine namba **DF4HL1701241,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**DAR/OST/RB/265471/2022**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Chama tawala Japan chapata ushindi

**TOKYO,** Japan

WAZIRI Mkuu wa Japan, Fumio Kishida, anajiandaa kuimarisha mamlaka ndani ya chama chake tawala baada ya kupata ushindi mkubwa katika uchaguzi uliofanyika jana.

Kishida alipata ushindi na kujihakikishia miaka mingine mitatu ya kuiongoza Japan kama waziri mkuu.

Chama hicho hata hivyo kinaomboleza kifo cha Shinzo Abe mtu aliyekuwa na ushawishi mkubwa wa kisiasa katika usimamizi wa madaraka na alikuwa na kundi kubwa ndani ya chama cha LDP.

Wachambuzi wanasema kifo chake huenda kikasababisha uwezekano wa kuweka mivutano ndani ya chama na inaweza kumpa changamoto Kishida katika uongozi. Chama cha LDP na mshirika wake mdogo Komeito walishinda viti 76 kati ya 125 vya bunge ikiwa ni ongezeko la viti bungeni ikilinganishwa na idadi ya 69 walivyokuwa navyo bunge lililopita.

Waziri Mkuu Kishinda amepata nafasi ya kupumua katika utekelezaji wa ajenda muhimu ambazo ni pamoja na kuongeza bajeti ya ulinzi na kuipitia upya katika ya nchi hiyo ambayo ilikuwa ni ndoto ya Shinzo Abe iliyowekwa pembeni kwa muda mrefu kabla ya kujiuzulu kwake kutokana na maradhi mnamo mwaka 2020. **DW**

## Wanajeshi 49 wa Ivory Coast wakamatwa Mali

**BAMAKO,** Mali

WANAJESHI 49 wa Ivory Coast wanaosemekana kuwa walikuwa wakijiunga na kikosi cha Umoja wa Mataifa nchini Mali (Minusma) wamekamatwa wakati wakiingia nchini humo.

Taarifa kutoka nchini humo, ilielezwa kukamatwa kwa wanajeshi hao inatokana na tuhuma ya kuweko kwa uvumi wa jaribio la mapinduzi.

Wanajeshi waliokamatwa inasemekana hawakuwa na kibali cha ujumbe wa Umoja wa Mataifa na wote walipakiwa ndani ya mabasi mawili madogo na kisha kusafirishwa. Tovuti ya Bamako iliripoti kuwa uwanja wa ndege kwa sasa umewekwa chini ya uangalizi mkali na wanajeshi kadhaa wa vikosi vya usalama.

Tovuti ya Maliactu ilisema katika chapisho la Facebook kwamba wanajeshi hao hawakuwa wamebeba silaha lakini walikuwa na mizigo chini ya uangalizi wa Minusma.

Tovuti ya Malijet ilisema kuwa vikosi maalum vya Mali vilitumwa kulinda uwanja wa ndege baada ya wanajeshi wa Ivory Coast kushindwa kutekeleza majukumu yao. **BBC**

# Russia yafunga bomba la gesi, Ujerumani sasa hofu tupu

**BERLIN,** Ujerumani

HATIMAYE Russia imelifunga bomba la kusafirisha gesi kwenda Ujerumani la Nord Stream 1, ikieleza kuwa inataka kulifanyia ukarabati.

Hata hivyo, Ujerumani imeonya hatua hiyo kuwa inaweza kuwa ya kudumu.

Ufungaji wa bomba hilo kimsingi itapunguza usambazaji wa gesi barani Ulaya, na baadhi ya maofisa wanaonyesha hofu kwamba huenda Russia itarefusha muda wa ukarabati kwa lengo kuondosha hali ya utulivu barani Ulaya ingawa mpango wa utelekezaji wa hatua hiyo ulikuwapo tangu awali.

Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Nishati wa Ujerumani, Klaus Müller amenukuliwa na shirika la habari la Uingereza la Reuters akisema kinachoweza kutokea baada ya kuhitimishwa ukarabari huo, hakuna anaweza kukizungumzia kwa sasa.

"Kwa sasa tayari, bili za watumiaji wa gesi zimepanda zaidi lakini ongezeko hilo lilianza katika vipindi vya vuli na baridi vilivyopita. Kuna tishio la ongezeko kubwa la bei ambalo waagizaji wa gesi tayari wanapaswa kulipa sasa," alisema.

**Gavana wa eneo hilo Oleh Syneihubov, kupitia ukurasa wake wa telegram alisema vikosi vya Russia vinashambulia maeneo ya raia.**

### JITIHADA YA KUPUNGUZA UTEGEMEZI

Ujerumani na mataifa mengine ya Ulaya yapo katika jitihada za kupunguza utegemezi wa uagizaji wa nishati kutoka Russia.

Ujerumani kwa mfano, taifa ambalo lina uchumi mkubwa barani Ulaya limekuwa likitumia asilimia 35 ya gesi kwa matumizi ya kiwanda na kuzalisha nishati ya umeme.

Mwezi uliopita makamu wa Kansela Robert Habeck alizindua awamu ya pili ya taifa lake ya jitihada ya mpango wa dharura wa hatua ya tatu katika usambazaji wa gesi, huku akionya kwamba kitovu cha uchumi wa Ulaya kinakabiliwa na janga na hasa katika hifadhi ya nishati yake kuelekea katika msimu wa baridi.

### MJI WA KHARKIV UNASHAMBULIWA

Nchini Ukraine majeshi ya Russia yameongeza mashambulizi yake katika mji wa pili kwa ukubwa wa taifa hilo Kharkiv, kwa lengo la kuongeza udhibiti katika miji ya mashiriki ya Ukraine.

Gavana wa eneo hilo Oleh Syneihubov, kupitia ukurasa wake wa telegram alisema vikosi vya Russia vinashambulia maeneo ya raia.

Aliyataja maeneo matatu yaliyovurumishiwa makombora ni shule, jengo la makazi na kombora la tatu lilitua karibu na eneo la ghala.

Mashambulizi hayo yametokea siku mbili tu baada ya shambulio la roketi la Russia kuvunja majengo ya ghorofa mashariki mwa Ukraine, na kusababisha vifo vya watu wasiopungua 19.

Safari ya mwisho ya Putin nje ya nchi yake ilikuwa ya nchini China mapema Februari, ambapo yeye na Rais wa China Xi Jinping walizindua mkataba wa urafiki usio na ukomo, muda mfupi kabla ya wote wawili kuhudhuria sherehe za ufunguzi wa michezo ya Olimpiki ya majira ya baridi. **DW**



Baadhi ya waandamanaji waliovamia Ikulu ya Sri Lanka wakiwa wamelala katika kitanda cha Rais Gotabaya Rajapaksa ambaye amekimbilia sehemu isiyojulikana. **PICHA: REUTERS**

# Sri Lanka iko katika ombwe la kisiasa

**COLOMBO,** Sri Lanka

KWA siku tatu nchi ya Sri-Lanka iko katika ombwe la kisiasa kufuatia viongozi wa upinzani kushindwa kukubaliana nani atachukua nafasi zilizoachwa na viongozi waliojiuzulu.

Waandamanaji nchini humo wanaendelea kukaa katika makazi na ofisi ya Rais Gotabaya Rajapaksa na kwenye makazi ya waziri mkuu tangu Jumamosi wakishinikiza viongozi hao waondoke madarakani na wameapa kuendelea kubakia hadi pale viongozi hao wanajiuzulu rasmi.

Waziri Mkuu Ranil Wickremesinghe, alisema kwamba ataachia ngazi pale serikali mpya itakapochaguliwa na saa chache baadaye spika wa bunge alitangaza kwamba Rais Rajapaksa ataondoka madarakani Jumatano na ameshathibitisha uamuzi huo.

Viongozi wa upinzani wamekuwa katika mazungumzo ya kuunda serikali mbadala itakayojumuisha vyama vyote na kiongozi mkuu wa upinzani Sajith Premadasa na Dulla Allahperuma aliyekuwa waziri chini ya Rajapaksa wamependekezwa kushika nafasi ya urais na waziri mkuu. Viongozi hao wameombwa kujadili watakavyogawana nafasi hizo kabla ya kukutana na spika wa bunge.

Aidha, mamilioni ya fedha za rupee zilizoachwa na Rais Gotabaya Rajapaksa nyumbani kwake baada ya kukimbia yatakabidhiwa mahakama. **DW**

# WAWA, MNATA MALI YA SINGIDA BIG STARS

Saada Akida na Adam Fungamwango

UONGOZI wa Singida Big Stars umefanikiwa kuwanasa beki wa Ivory Coast, Pascal Wawa na golikipa wa Polisi Tanzania, Metacha Mnata tayari kwa ajili ya msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wawa amesaini mkataba wa miaka miwili kuitumikia timu hiyo akitokea Simba baada ya kumaliza mkataba na Wekundu wa Msimbazi hao kwa msimu huu ulioisha.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Muhibu Kanu, amesema kuwa mawindo ya kusaka saini za wachezaji wengine bado yanaendelea.

**Alisema usajili wa wachezaji wa kigeni wameanza na Wawa na baada ya hapo wako katika mchakato wa kumalizana na wabrazili wanne, wakiwamo kiungo na mshambuliaji.**

"Ni kweli tumemalizana na Wawa na sasa tuko katika mazungumzo na wachezaji wanne wa kigeni ambao wanatoka Brazil, viungo na washambuliaji kwa ajili ya kuimarisha kikosi chetu kwa msimu mpya," alisema Kigogo huyo.

Metacha ambaye anaichezea timu ya taifa, Taifa Stars ametambulishwa rasmi kwenye mtandao wa kijamii wa klabu hiyo.

"Rasmi, Metacha Mnata ni Big Star," iliandika akaunti ya Instagram ya klabu hiyo.

Kujiunga kwa kipa huyo kunaongeza idadi ya wachezaji waliosajiliwa wa klabu hiyo inayokwenda kucheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu ujao, baada ya kupanda daraja kwa la DTB, ambalo lilibadilishwa baada ya kutinga Ligi Kuu.

Wachezaji ambao tayari wameshatia wino kwenye kikosi hicho hadi sasa ni Kelvin Sabato kutoka Mtibwa Sugar, Abdulmajid Mangalo kutoka Biashara United, Paul Geofrey kutoka Yanga, na Aziz Andambwile aliyetokea Mbeya City.

Awali kabla ya kutua Polisi Tanzania, Metacha alikuwa anaichezea Yanga na ilibaki kidogo asajiliwe kwenye kipindi cha dirisha dogo msimu uliomalizika, lakini ilishindikana.




Mkurugenzi Mtendaji wa MultiChoice Tanzania, Jacqueline Woiso (katikati), akifurahi pamoja na washiriki wa filamu za Mvamizi na Uncle za chaneli ya Maisha Magic Movies zilizotwaa tuzo katika Tamasha la Kimataifa la Filamu Zanzibar ZIFF hivi karibuni. Washiriki hao walitembelea ofisi za DStv Tanzania kutambulisha tuzo zao. Kutoka kushoto ni Mhitimu wa Akademi ya MultiChoice Talent Factory ambaye ni mzalishaji wa filamu ya Mvamizi, Philipo Ngonyani, mwigizaji wa filamu ya Uncle Tunu Mbegu, mwigizaji wa filamu ya Uncle Jaalia Ngonde na mzalishaji wa filamu ya Uncle Khatibu Madudu. Filamu zote hizo zilifadhiliwa na MNet. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Azam yachukua kocha mpya Hispania*

Na Saada Akida

MTENDAJI Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', amesema katika kuhakikisha wanaboresha timu yao na kuongeza nguvu ndani ya benchi la ufundi, wamemwajiri kocha mpya wa viungo, Mikel Guillen kutoka Hispania.

Akizungumza na gazeti hili jana, Popat alisema wanaendelea kuimarisha timu yao kila sehemu ikiwamo usajili pamoja na kuboresha benchi la ufundi kwa kuongeza nguvu.

Alisema Guillen ana uzoefu wa kufundisha timu za Aris Limassol ya Cyprus, inayoshiriki Ligi ya Europa Conference, Bengaluru ya India na Dinamo Bucuresti ya Romania.

"Uzoefu wake umemfanya kufundisha baadhi ya wachezaji wakubwa, akiwamo Sunil Chhetri, mfungaji namba sita wa mabao duniani kwa upande wa timu za Taifa, tunaimani atatusaidia kwa msimu ujao," alisema Popat.

Alisema msimu huu wamejipanga vizuri katika kila eneo kuanzia usajili kwa ajili ya kuimarisha timu yao kufikia mipango walijiwekea kwa msimu ujao kufanya vizuri, kutwaa mataji wanaokwenda kushiriki.

Mtendaji huyo alisema kulingana na mahitaji ya kikosi chao kiwe imara zaidi, kupata kocha wa viungo ni kuhakikisha wachezaji wao wanakuwa fiti zaidi.

# Shamsa: Wasanii wasiigize maisha

Na Sabato Kasika

MSANII nyota wa Bongo Movie, Shamsa Ford, amewataka wasanii wenzake kuishi maisha ya uhalisi kulingana na kipato chao badala ya kutaka sifa kwa watu kwa kujionyesha na wana pesa huku wakiumia.

Amesema, baada ya kuuza gari yake kutokana na changamoto za maisha, alikaa miaka miwili bila kuwa na gari, huku akitumia usafiri wa taksi na bajaj na kwamba hakusononeka kwa kuwa maisha ndivyo yalivyokuwa.

"Sikulazimisha kukodi magari kwa ajili ya kujionyesha kwa watu kuwa niko vizuri, nilibeba matatizo yangu na kupambana nayo mwenyewe kwani huo ndiyo ulikuwa uhalisia," amesema Shamsa.

Katika mtandao wake wa kijamii, ameandika kuwa, kuna wakati alikuwa na mtoto wake kwenye bajaj, huku mtoto huyo akimuuliza kuwa atapata lini gari, na pia akawa anamuomba apige picha akiwa katika magari ya watu wengine.

"Siku nyingine nilimsikia akisali akisema Mungu mpe gari mama yangu, ambapo Mungu amenisaidia nimepata gari ambayo inawezekana isiwe ya thamani, lakini ninaithamini sana," amesema.

Msanii huyo amesema, Mungu amemjalia amepata gari hiyo, na kwamba inamsaidia katika usafiri ambapo anawataka wasanii wenzake wajifunze kutolazimisha kumiliki vitu vikubwa hawana uwezo navyo.

"Lakini wasifananishe maisha yao na watu wengine ili waishi kwa amani, vinginevyo wanaweza kuaibika kwa kuishi maisha ya kuigiza kwa kuonyesha kuwa wanamiliki vitu fulani na kumbe sivyo," amesema.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**KANE KUMRITHI LEWANDOWSKI**

KLABU ya Bayern Munich inamsaka mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane, 28, kama mbadala wa Robert Lewandowski, 33, kutoka Poland anayetaka kuachana na mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, msimu huu. ***(Kicker)***

**PSG YAMTAKA LEWANDOWSKI**

CHELSEA na Paris St-Germain nazo zitaingia kwenye mbio za kutaka saini ya Robert Lewandowski kama itashindikana kujiunga na Barcelona. ***(Mail)***

**SILVA KUTUA BARCA**

KLABU ya Barcelona inaamini itamsajili kiungo Mreno, Bernardo Silva mwenye umri wa miaka 27 kutoka Manchester City. ***(Mundo Deportivo)***

**RONALDO NA CHELSEA**

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel ameweka ngumu kwa mshambuliaji wa Manchester United na Ureno, Cristiano Ronaldo, 37, kutua Stamford Bridge msimu huu. ***(Mail)***

**KLUIVERT AWINDWA**

KLABU ya West Ham imeelekeza macho yake kwa winga wa AS Roma na Uholanzi, Justin Kluivert, 23, baada ya kumkosa Arnaut Danjuma, 25, kutoka Villareall. ***(Gazzetta dello Sport)***

**KOULIBALY HUYO CHELSEA**

CHELSEA inajiandaa kukubaliana na ada wanayotaka Napoli ya pauni milioni 34 kwa ajili ya mlinzi wake wa kati raia wa Senegal, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 31. ***(Corriere dello Sport, via Sun)***

**JUVE YAMWANIA KOULIBALY**

JUVENTUS inatarajia kupata fedha za kuwezesha usajili wa Kaliodou Koulibaly kutokana na ada ya pauni milioni 90 wanayotarajia kupata kwa kumuuza mlinzi wao, Matthijs de Ligt mwenye umri wa miaka 22 anayesakwa na Bayern Munich na Chelsea. ***(Tuttosport)***

**PICKFORD NA MKATABA**

KLABU ya Everton inatarajia kumpa mkataba mpya kipa wake raia wa England, Jordan Pickford mwenye umri wa miaka 28. ***(Liverpool Echo)***

**GRIMALDO ATAKIWA**

ARSENAL iko kwenye mazungumzo na Benfica baada ya kupeleka ofa ya pauni milioni 6.4 kwa ajili ya kumsajili beki wa kushoto, Alex Grimaldo mwenye umri wa miaka 26. ***(Express)***

**CITY KUSAJILI BEKI**

KLABU ya Manchester City itasajili beki mpya wa kati msimu huu kama mlinzi, Nathan Ake mwenye umri wa miaka 27, atajiunga na Chelsea. ***(Fabrizio Romano)***

**PAQUETA AGOMBEWA**

ARSENAL na Newcastle zinamtaka kiungo mshambuliaji wa Lyon na Brazil, Lucas Paqueta, lakini ada ya pauni milioni 65 inayotakiwa na Wafaransa hao kwa ajili ya nyota huyo mwenye miaka 24 inaonekana ni maji marefu. ***(CBS Sports)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MAN UNITED SASA KUMTEMA RONALDO

**Yaeleza haiwezi kuendelea kuwa na mchezaji ambaye hataki kuwepo hapo na...**

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United iko tayari kumuacha Cristiano Ronaldo katika ziara yake ya kujiandaa na msimu mpya, iwapo nyota huyo hatajiunga na timu hiyo mwishoni mwa wiki hii, lakini wanatumaini Christian Eriksen atajiunga na kikosi kule Australia kwa wakati.

Ronaldo amebakia nchini Ureno na familia yake baada ya kupewa ruhusa ya kukosa mechi ya kwanza ya maandalizi ya msimu kwenye ziara ya Bangkok, Thailand ambapo United leo Jumanne itacheza na itamenyana na Liverpool.

**Klabu hiyo itakwenda Melbourne na Perth kesho Jumatano, na inakubali kuwa haitakuwa na maana kuendelea na Ronaldo kama hayuko tayari kurejea wiki hii.**

United wana matumaini kwamba, Eriksen atasaini kama mchezaji huru kwa wakati ili kujiunga na ziara hiyo nchini Australia baada ya kufanyiwa vipimo vya afya.

Mazungumzo yanaendelea kuhusu mchezaji anayelengwa na United, Frenkie de Jong licha ya utata wa uhamisho wake kutoka Barcelona na madai ya Mholanzi huyo kwamba anataka kusalia Nou Camp.

Klabu hizo mbili zimefikia makubaliano mapana juu ya mkataba wa pauni milioni 55, lakini Barca bado wanadaiwa pauni milioni 17 zaidi ili kumuachia De Jong.

United watakuwa na matumaini ya kukamilisha uhamisho haraka iwezekanavyo huku wakitarajia kujenga upya kikosi chao.

Beki Tyrrell Malacia tayari amewavutia mashabiki wa United kutokana na video za mazoezi na habari za Eriksen zilipokelewa vivyo hivyo.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT
TZS. 281,

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
LIVERPOOL
1 | 3.55
X | 3.79
2 | 1.80

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# RAPHINHA AKARIBIA KUTUA CHELSEA

**BARCELOBA,** Hispania

KLABU ya Barcelona inakaribia kumsajili kiungo wa kati wa Leeds United, Raphinha kwa bei ya jumla ya pauni milioni 63.

Barcelona imekuwa mahali anapopendelea zaidi Mbrazili huyo, lakini hadi hivi majuzi Chelsea ndio ilikuwa timu pekee iliyofikia thamani ya Leeds ya pauni milioni 55, pamoja na nyongeza ya pauni milioni 8.

Hata hivyo, nyota huyo sasa ana nafasi kubwa zaidi ya kutua kule Nou Camp na kuna uwezekano kwamba mchezaji huyo atakamilisha ndoto yake.

Habari hizo zitakuja kuwa pigo kwa Kocha wa Chelsea, Thomas Tuchel, ambaye anakaribia kukamilisha dili la kumsajili Raheem Sterling kutoka Manchester City.

Mchezaji huyo wa England alikuwa jijini London kwa ajili ya kufanyiwa vipimo vya afya na anatazamiwa kujiunga na Chelsea kule Los Angeles, Marekani, ambako wako kwenye ziara ya maandalizi ya msimu mpya.

Beki wa Man City, Nathan Ake yuko tayari kumfuata Sterling na kurejea Stamford Bridge.

Matatizo ya kifedha - ikiwa ni pamoja na deni lililoripotiwa la pauni milioni 508 yalionekana kama kuwa kizuio cha Barcelona kumnasa Raphinha, lakini sasa ni wazi kwamba mchezaji huyo anaelekea kule Katalunya.



## Rooney atajwa kocha mpya DC Utd

**NEW YORK,** Marekani

KLABU ya DC United imemteua Wayne Rooney kama kocha wao mpya, kwa mujibu wa Daily Mail.

Rooney aliondoka katika klabu ya ligi daraja la kwanza ya Derby, Juni, baada ya kupitia kipindi kigumu katika kazi yake ya kwanza kama kocha.

Akiwa ameibeba Derby katika siku ya mwisho ya msimu wa 2020-21, Rooney hakuweza kurudia jambo hilo muhula uliopita, kwa sehemu kubwa kutokana na adhabu ya kukatwa pointi 21 kwa matumizi mabaya ya fedha na umiliki wao.

Alikuwa akivutiwa na klabu yake ya zamani ya Everton, Januari, lakini alikataa nafasi ya kuhojiwa na nafasi yake ikajazwa na Frank Lampard.

Rooney sasa anatazamiwa kuchukua mikoba ya DC inayoshiriki Ligi Kuu ya Soka ya Marekani, ambako alicheza mwaka wa 2018 na 2019 kabla ya kurejea England kujiunga na Derby.

Mwandishi wa Athletic, Pablo Iglesias Maurer aliripoti Jumapili kwamba masharti kati ya DC na Rooney ambaye ni mfungaji bora wa Manchester United - yamekubaliwa.

Rooney alifunga mabao 25 katika mashindano yote akiwa na klabu hiyo ya Marekani baada ya kujiunga nayo mwaka 2018 akitokea Everton.

## HABARI MICHEZO


# 620,910 JACKPOT

## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 13/07/22 | 19:30 | Ismaily SC vs Smouha Club | 2.48 | 3.01 | 2.96 |
| 02. 13/07/22 | 20:00 | Dinamo Batumi vs Slovan Bratislava | 2.56 | 3.06 | 2.76 |
| 03. 13/07/22 | 20:00 | Shakhter Soligorsk vs Maribor | 2.66 | 3.06 | 2.66 |
| 04. 13/07/22 | 21:45 | Linfield Belfast vs The New Saints | 2.30 | 3.15 | 3.05 |
| 05. 14/07/22 | 01:00 | Goias vs Atletico GO | 2.74 | 2.93 | 2.54 |
| 06. 14/07/22 | 02:00 | Ceara CE vs Fortaleza CE | 2.41 | 2.85 | 2.99 |
| 07. 14/07/22 | 03:00 | Inter Miami CF vs Philadelphia Union | 2.70 | 3.36 | 2.55 |
| 08. 14/07/22 | 03:30 | Santos vs Corinthians | 2.35 | 2.94 | 2.99 |
| 09. 14/07/22 | 04:00 | FC Dallas vs New York City | 2.53 | 3.57 | 2.60 |
| 10. 14/07/22 | 18:00 | College Europa vs Vikingur Gota | 2.37 | 3.33 | 2.88 |
| 11. 14/07/22 | 18:00 | Ararat Yerevan vs Shkendija | 2.29 | 3.37 | 2.97 |
| 12. 14/07/22 | 19:00 | Milsami Orhei vs FK Panevezys | 2.78 | 3.18 | 2.53 |
| 13. 14/07/22 | 19:00 | Seinajoen JK vs Flora Tallinn | 2.82 | 3.23 | 2.46 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE - 12/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1026 | Shanghai SIPG vs Wuhan Three Towns FC | 4.92 | 3.83 | 1.57 |
| 14:30 | 2293 | Tianjin Teda vs Shijiazhuang | 2.01 | 3.19 | 3.44 |
| 15:00 | 3531 | Madagascar vs Namibia | 2.22 | 2.75 | 3.49 |
| 16:00 | 2442 | Shakhter Karagandy vs Aksu | 1.85 | 3.28 | 3.92 |
| 16:00 | 3571 | Manchester Utd vs Liverpool | 3.55 | 3.79 | 1.80 |
| 17:30 | 2330 | National Bank vs Ghazl EL Mahallah | 2.13 | 3.01 | 3.66 |
| 18:00 | 3102 | FK Arys vs Aktobe | 3.78 | 3.00 | 1.99 |
| 18:00 | 5694 | Froya Fotball vs Skeid Fotball 2 | 3.92 | 4.21 | 1.65 |
| 18:30 | 2562 | Ilves 2 vs HJS Akatemia | 2.31 | 3.73 | 2.50 |
| 18:30 | 4495 | Rigas Futbola Skola vs HJK Helsinki | 2.25 | 3.20 | 3.10 |
| 19:00 | 1963 | Denmark W vs Finland W | 1.35 | 4.41 | 7.45 |
| 19:00 | 2401 | Karabakh vs Lech Poznan | 1.81 | 3.40 | 4.30 |
| 19:00 | 3622 | Lincoln FC vs Shkupi Skopje | 3.16 | 3.31 | 2.17 |
| 19:00 | 4745 | Zalgiris vs KF Ballkani | 1.81 | 3.39 | 4.28 |
| 19:30 | 2649 | Zamalek vs Arab Contractors | 1.55 | 3.81 | 6.02 |
| 19:30 | 4666 | Talaea El Gaish vs Pyramids | 4.52 | 3.06 | 1.90 |
| 20:00 | 1157 | Kongsvinger 2 vs Lillehammer FK | 2.11 | 4.31 | 2.55 |
| 20:00 | 1930 | Sheriff Tiraspol vs Zrinjski Mostar | 1.75 | 3.34 | 4.79 |
| 20:00 | 2535 | Orebro SK vs Trelleborgs FF | 2.25 | 3.46 | 3.06 |
| 20:00 | 3946 | Landskrona Bois vs Halmstads BK | 3.93 | 3.52 | 1.92 |
| 21:00 | 1534 | Sandefjord vs Aalesunds | 2.56 | 3.41 | 2.56 |
| 21:00 | 2143 | KF Tirana vs Dudelange | 1.86 | 3.30 | 4.20 |
| 21:00 | 4897 | Hibernians vs Shamrock Rovers | 4.40 | 3.65 | 1.73 |
| 21:00 | 5016 | KI Klaksvik vs Bodo Glimt | 4.60 | 4.00 | 1.63 |
| 21:00 | 5898 | KF Drita vs Inter Turku | 2.36 | 3.17 | 3.02 |
| 21:45 | 1053 | Hamilton vs Stranraer | 1.38 | 4.51 | 6.47 |
| 21:45 | 1804 | Fraserburgh vs Montrose | 4.33 | 3.89 | 1.63 |
| 21:45 | 2059 | Albion Rovers vs Cove Rangers | 9.40 | 5.88 | 1.21 |
| 21:45 | 2354 | Queens Park vs Forfar Athletic | 1.60 | 3.84 | 4.63 |
| 21:45 | 3113 | Falkirk FC vs Hibernian | 13.68 | 6.26 | 1.15 |
| 21:45 | 3549 | St Johnstone vs Annan Athletic | 1.21 | 5.72 | 9.87 |
| 21:45 | 3590 | Dunfermline vs Buckie Thistle FC | 1.38 | 4.51 | 6.47 |
| 21:45 | 3680 | Ayr United vs Queen of South | 1.75 | 3.58 | 4.02 |
| 21:45 | 3696 | Alloa Athletic vs East Fife | 1.73 | 3.72 | 3.92 |
| 21:45 | 5125 | Livingston vs Inverness | 1.96 | 3.29 | 3.49 |
| 21:45 | 5689 | Airdrieonians vs Edinburgh City | 1.62 | 3.94 | 4.33 |
| 22:00 | 2351 | Germany W vs Spain W | 2.84 | 3.23 | 2.28 |
| 22:00 | 3868 | Al Ahly Cairo vs Coca Cola | 1.51 | 4.03 | 6.05 |
| 22:00 | 4510 | Sutjeska vs Ludogorets Razgrad | 6.42 | 4.51 | 1.42 |
| 22:30 | 5949 | Vikingur Reykjavik vs Malmo | 4.41 | 3.81 | 1.69 |
| 23:00 | 1181 | Deportivo Tachira vs Metropolitanos | 2.02 | 3.09 | 3.54 |
| 23:00 | 3817 | Zulia FC vs Carabobo FC | 2.70 | 2.85 | 2.80 |

### JUMATANO - 13/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 4105 | Uruguay W vs Brazil W | 59.11 | 12.81 | 1.01 |
| 00:10 | 4202 | Los Andes vs Talleres RDE | 3.10 | 2.76 | 2.41 |
| 02:00 | 1494 | Alianza Petrolera vs Union Magdalena SM | 1.73 | 3.33 | 4.50 |
| 02:00 | 4944 | North Carolina FC U23 vs Charlotte Eagles | 2.29 | 4.50 | 2.38 |
| 02:30 | 3927 | Atletico Pr vs Bahia BA | 1.69 | 3.34 | 4.81 |
| 03:00 | 2784 | Argentina W vs Peru W | 1.13 | 6.70 | 14.77 |
| 03:00 | 4242 | Cruzeiro vs Fluminense | 2.51 | 2.85 | 2.85 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# MICHUANO YA KUAMBIANA CUP YARINDIMA LUDEWA

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, amewataka vijana kujihusisha na michezo mbalimbali ikiwamo mpira wa miguu ili kuweza kujipatia kipato na kuboresha afya zao.

Hayo ameyasema wilayani Ludewa mkoani Njombe alipokuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa mashindano ya mpira wa miguu msimu wa tatu yajulikanayo kama Kuambiana Cup ambayo huandaliwa na Imani Haule yakihusisha kata 5 za tarafa ya Masasi chini ya udhamini wa Kuambiana Investment yakiambatana na kauli mbiu isemayo "Mtu kwao rejesha furaha nyumbani".

Aidha kwa upande wa mwandaaji wa mashindano hayo Imani Haule (Kuambiana) ambaye ni mkurugenzi wa Kuambiana Investment amesema mashindano hayo yamekuwa na matokeo mazuri na amewaomba wadau mbalimbali kujitokeza kuunga mkono wachezaji hao katika suala zima la usafiri ili vijana hao waweze kutimiza ndoto zao.

**"Vijana wengi wanahitaji kushiriki michezo hii, lakini changamoto iliyopo ni usafiri wa kutoka vijijini kwao na kuwafikisha katika eneo la mashindano, hivyo nawaomba wadau mbalimbali wajitokeze kuwaunga mkono vijana hawa ili waweze kusafirishwa," alisema Haule.**

Ameongeza kuwa yeye ni mzaliwa wa Wilaya ya Ludewa, hivyo amekuwa anatamani kuona vijana kutoka maeneo hayo wakipata nafasi za kuchezea timu kubwa hapa nchini.

Naye Sunday Deogratius ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, amempongeza Kuambiana kwa kukumbuka vijana wa nyumbani kwao kwa kuwa watu wengi wamekuwa wakisahau kuinua wengine waliobaki nyuma.

Mashindano hayo yanafanyika ikiwa ni msimu wa tatu toka kuanzishwa kwake mwaka 2020 na Masasi ya wilaya ya Ludewa iliibuka mshindi kwa kuifunga Polisi Nyasa 3-1 na kujipatia fedha kiasi cha Sh. 300,000, kombe pamoja na medali.




Mshindi wa Jackpot bonus, Paul Niwa Maguhu (38) kutoka Arusha akishikilia mfano wa hundi ya Sh. 7,718,797 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 15 kati ya 17 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. **PICHA : MPIGAPICHA WETU**

# *Coastal yaanza kutengeneza Sopu wengine*

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumsajili straika wa KMKM ya Zanzibar, Optatus Lupekenya, klabu ya Coastal Union imesema huu ndiyo wakati wa kusajili na kutengeneza wachezaji wengine kama kina Abdul Selemani 'Sopu'.

Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili wa klabu hiyo amesema baada ya kuondoka Sopu na Victor Akpan, klabu haipaswi kulia, badala yake imeanza kufanya usajili na itawatengeneza wachezaji wengine kama hao, ili nao pia watamaniwe na klabu zingine baada ya msimu ujao.

"Dunia ya sasa ya mpira unanunua na kuuza, unanunua kwa bei ya kawaida na kuwatengeneza, halafu unauza kwa bei kubwa, kwa hilo tumefanikiwa na kupiga hatua nzuri, japo kuna mengine makubwa yanakuja," alisema Aurora.

Alisema pamoja na kuwauza wachezaji hao, mkulima hawezi kula mbegu zake mwenyewe, hivyo wanakwenda kufanya usajili wa maana kwa Watanzania wenye vipaji kwa maelekezo ya Kocha Mkuu, Juma Mgunda.

"Sisi kama wakulima, hatuwezi kula mbegu zetu wenyewe, tunatengeneza timu nzuri zaidi ya msimu huu, tutaanza kusajili wachezaji wa nyumbani kwenye vipaji kama mlivyomuona Sopu. Kama tutashindwa kupata wachezaji ambao tunawahitaji kufanya vema kwenye baadhi ya maeneo, basi tunatoka kwenda kusajili nje, lakini wengi watakuwa wa ndani," alisema mwenyekiti huyo.

Coastal imewauza wachezaji wawili kwa mpigo, Sopu aliyenyakuliwa na Azam, huku Mnaigeria, Akpan aliyejiunga na Simba.

Misimu miwili nyuma, klabu hiyo iliwatoa, Bakari Mwamnyeto aliyekwenda Yanga na Ibrahim Ame, aliyechukuliwa na Simba.

# Michezo

Jumanne Julai 12, 2022

Nipashe




Man United kumtema Ronaldo

UKURASA 21



Mhandisi Ujenzi wa Manispaa ya Kinondoni, Issac Mpaki (kushoto), akimwonyesha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ramani ya Uwanja wa Timu ya KMC utakaojengwa Mwenge, jijini Dar es Salaam, alipofanya ziara katika mkoa huo jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Simba yamaliza ndani, kushusha vyuma vya nje*

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Leo inaanza kutangaza wachezaji wa kimataifa ambao imewasajili, huku...

KLABU ya Simba jana ilimaliza kutangaza wachezaji wa ndani iliowasajili kwa msimu ujao wa ligi, baada ya kumtambulisha rasmi Nassor Kapama aliyetokea Kagera Sugar na kuanzia leo inatarajiwa kuanza kuwaweka hadharani wachezaji wa kimataifa iliyowasajili kutoka nje ya nchi.

**Kapama alitambulishwa jana mchana kwenye mtandao rasmi wa klabu hiyo, huku Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally akisema kuwa huyo anakuwa mchezaji wa mwisho kutangazwa, na kuanzia leo itaanza kuweka hadharani wachezaji iliyowasajili kutoka nje ya nchi.**

"Tumemaliza wachezaji wa ndani, Kapana ndiye mchezaji wa mwisho wa Kitanzania, kuanzia kesho Jumanne (leo) tunaanza kushusha vyuma vya wachezaji mbalimbali kutoka barani Afrika, huko sasa ndiyo bahari, balaa zito linakwenda kufanyika. Tumesajili watu wa maana kweli kweli, leo mtaanza kuona vyuma," alisema Ahmed.

Tayari Simba imewatambulisha wachezaji wawili wazawa, ikiwa na maana kuwa imesajili idadi hiyo kwa Watanzania msimu huu, ambao mbali na Kapama, mwingine ni Habib Kyombo akitokea Mbeya Kwanza.

Huyo anakuwa ni mchezaji wa tatu kutangazwa na Simba kwa siku tatu mfululizo na wa nne hadi sasa.

Kyombo, Mnaigeria Victor Akpan walitangazwa kwa kupishana siku moja moja, huku Moses Phiri raia wa Zambia kutoka Zanaco ya huko alikuwa mchezaji wa kwanza kutangazwa, ikiwa ni idadi ya wachezaji wanne mpaka sasa kuwekwa hadharani.

Kapama, straika wa zamani wa Ndanda, ana uwezo wa kucheza nafasi nyingi uwanjani, kwani alipohamia Kagera Sugar alikuwa akicheza pia kama kiungo mkabaji, wakati mwingine beki, huku pia akiwa na uwezo wa kucheza nafasi yake ya asili ya ushambuliaji.

Ahmed alisema wakati wakianza kuwatambulisha mchezaji mmoja mmoja kutoka nje kuanzia leo, mpaka sasa ni mchezaji mmoja tu aliyeachwa, naye ni Paschal Wawa.

Hata hivyo, alisema kwa sasa wanaendelea na mazungumzo na baadhi ya wachezaji kwa ajili ya kuvunja nao mikataba.

"Kuna wachezaji tunataka kuachana nao, lakini bado wana mikataba, kwa hiyo tuko kwenye mazungumzo nao kwa sababu hatutaki tuachane halafu tuanze kukimbizana FIFA kwa ajili ya kudaiana, tumalizane tuachane kwa amani," alisema.

# Yanga yakutana kuweka mikakati kimataifa

**Na Saada Akida**

UONGOZI mpya wa Yanga sasa unakutaka kwa ajili ya kuhakikisha wanaingia kwa kasi mpya kuhakikisha wanapanga mikakati yao ya kujiandaa na kuweka rekodi ya kuifanya kuwa timu ya kwanza kubeba ubingwa wa Afrika.

Yanga imebeba mataji matatu msimu wa 2021/22 ikiwa ni Ligi Kuu Bara, Kombe la Shirikisho (FA) na Ngao ya Jamii, na itashiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu.

Akizungumza na gazeti jana rais wa Yanga, Injinia Hersi Said alisema baada ya kumalizika kwa mchakato wa uchaguzi na kupata uongozi mpya watakutana kwa ajili ya kupanga mikakati yao ya kujiimarisha katika michuano ya kimataifa.

Alisema anataka kuona ndani ya kipindi cha uongozi wake, kupambana na kuhakikisha wanafanikiwa malengo yao ya kufanya vizuri na inawezekana kutokana na mikakati atakayoiweka ikiwamo kusuka kikosi imara cha wachezaji bora wa kiwango kizuri.

"Ninataka kuona timu ya Yanga inaweka rekodi ya kufanya vizuri katika michuano ya Afrika na hilo linawezekana kwetu, kwa sasa kila timu itaangalia michuano ya kimataifa kutokana na usajili ambao tumeufanya wa kutikisa Afrika," alisema Hersi.

Alisema mikakati yao ni kuhakikisha wanafanya vizuri katika michuano hiyo, wakianzia suala la usajili wa wachezaji wa kigeni kupata vibali vya kufanikisha nyota hao kucheza michuano hiyo.

"Tumefanya usajili baadhi ya wachezaji akiwamo Morrison (Bernard) na Kambole (Lazarous) na Gael Bigirimana kuwa ingizo jipya ndani ya kikosi cha Yanga, tunaendelea kuweka mikakati yetu kuelekea katika michuano ya kimataifa kwa kufanya vizuri ikiwezekana kufika robo au ubingwa Afrika," alisema Hersi.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >